# Nipashe

Jumamosi Februari 4, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581211

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


SUPA JACKPOT
TZS. 1,072,549,524
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




## Kinyang'anyiro Askofu Mkuu wa Anglikana chapamba moto

UKURASA 3

ULAWITI SHULENI

# Ripoti timu ya uchunguzi yaiva



Prof. Adolf Mkenda

• **Namba** maalum kuripoti yatangazwa, vitabu vyenye 'madudu' marufuku...*uk. 2*



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (wa pili kulia), akimimina mboga kwenye sinia la ubwabwa wakati wakipata chakula cha mchana kwa mama lishe katika kijiji cha Kinole, wakati wa ziara wilayani Morogoro jana. Wengine ni Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, Shabani Taletale 'Babu Tale' (kulia), Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema (kushoto), Katibu wa NEC na Oganaizesheni, Issa Gavi na wananchi wengine. **Habari Uk. 04.** **PICHA: MARY GEOFREY**

UKURASA 10

# Marufuku kuingiza ndizi Zanzibar



Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Shamata Shaame Khamis, akikagua shehena ya ndizi mbivu zilizokamatwa bandarini Zanzibar jana zikitokea Tanzania Bara, zilizoingizwa na mfanyabiashara Veronica Manjala (hayuko pichani) kutokana na Zanzibar kupiga marufuku uingizaji wa ndizi baada ya kuibuka ugonjwa wa migomba kusinyaa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mbunge: Mfumo uteuzi mawaziri ubadilishwe

UK.2


**MICHEZO** YANGA, NAMUNGO HESABU ZITAAMUA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu akipokea ujumbe maalum kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Kenya, William Ruto, uliowasilishwa na Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda wa nchi hiyo, Moses Kuria, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. Ujumbe huo ulilenga zaidi kwenye kuongeza na kudumisha undugu na pia ushirikiano wa Kiuchumi na Kibiashara. **PICHA: IKULU**

# Ripoti ulawiti shuleni yaiva

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RIPOTI ya timu maalum iliyoundwa na serikali kuchunguza taarifa za kuwapo tatizo la wanafunzi kufundishwa vitendo vya ulawiti kwenye baadhi ya shule mkoani Kilimanjaro, inatarajiwa kutangazwa hivi karibuni.

Timu hiyo iliundwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ikiongozwa na Kamishna wa Elimu nchini baada ya Nipashe kuripoti kuwapo shule zinazofundisha masuala hayo mkoani humo kinyume cha maadili ya kitanzania.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Francis Michael alisema kutokana na mambo hayo, wizara imekuja na kituo cha huduma kwa wateja na namba maalum ili watanzania watoe taarifa kwa wakati na zifanyiwe kazi.

"Lengo la kituo hiki ni kama kuna mtanzania atapata taarifa ya jambo lolote linalokwenda kinyume cha maadili, miongozo na taratibu za elimu nchini kwetu, aweze kutoa taarifa ili kuzipata kwa wakati na kufanyia kazi," alisema.

Katibu Mkuu alisema wizara imeandaa kituo hicho kitakachopokea taarifa na kitakuwa wazi kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 10 jioni.

"Mtanzania yeyote ambaye ataona jambo ambalo si jema ambalo linakiuka miongozo, maadili na tamaduni zetu kwenye taasisi zetu za elimu kwa shule za msingi, sekondari hadi vyuoni, atatutaarifu kwa kutumia namba hizi ambazo ni 0262160270, hii ni ya mezani na ya mkononi ni 0737962965," alisema.

Alibainisha kuwa kituo hicho kitapokea taarifa zote zinazohusu ukiukwaji wa taratibu na miongozo ya utoaji wa elimu kwenye taasisi za elimu sambamba na matukio ya ukatili na uvunjifu wa maadili kwa watoto shuleni.

"Mtu yeyote atakayetoa taarifa, zitakuwa ni siri na mtoaji hatabainika na atalindwa kwa mujibu wa sheria. Watanzania wawe huru kutoa taarifa ili tukinga na kumlinda mtoto wa kitanzania," alisema. Akizungumzia vitabu visivyo na maadili, Katibu Mkuu huyo alisema wizara imebaini kuna baadhi ya shule ambazo zimekuwa zikiingiza na kutumia vitabu ambavyo maudhui yake yanakinzana na mila, desturi, miongozo na tamaduni za mtanzania.

"Baadhi ya vitabu hivyo vimekuwa na hadithi ambazo maudhui yake yanahatarisha ukuaji wa malezi ya mwanafunzi na kupotosha mila na desturi za nchi yetu katika makuzi na malezi ya watoto wa kitanzania," alisema.

Mtendaji huyo wa wizara alisema vitabu hivyo visivyostahili kutumika, orodha yake itatangazwa na Waziri wa Elimu kupitia ripoti na kuvipiga marufuku.

"Niwakumbushe wamiliki na waendeshaji wa shule binafsi na za umma zilizosajiliwa nchini, kufuata na kuzingatia waraka namba nne wa mwaka 2014 pamoja na sheria na miongozo izingatiwe, vinginevyo hatua kali hadi za kufungia usajili shule hiyo zitachukuliwa," alisema.

Alisema kuwa waraka huo, pamoja na mambo mengine, unaelekeza njia za ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia ubora na maslahi ya nchi, mila, desturi za kitanzania.

Alisema waraka huo pia unalenga kuhakikisha vitabu vya ziada na kiada vinavyotumika kwenye shule zilizosajiliwa nchini, yaani zinazotumia mtaala wa ndani na zile zinazotumia mtaala wa nje, zitumie vitabu vinavyozingatia mila, desturi na utamaduni wa nchi na kulinda mtoto wa kitanzania aliyepo shuleni.

# Mpina ataka mfumo uteuzi wa mawaziri ubadilishwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina ameitaka serikali kubadili mfumo kwa baadhi ya ajira za viongozi ikiwamo Mawaziri zinazopatikana kwa uteuzi ziwe za ushindani ili kupata viongozi wasiotiliwa shaka.

Akiuliza maswali ya nyongeza bungeni jana, Mpina alihoji: "Kwanini serikali isiachane na baadhi ya ajira kupatikana kwa uteuzi badala yake ajira zote zipatikane kwa ushindani ajira za viongozi, ajira za watendaji, mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi ili kuiwezesha serikali kupata viongozi wenye uwezo usiotiliwa shaka katika nafasi mbalimbali za serikali."

Pia alihoji mkakati wa dharura wa serikali kudhibiti biashara holela, uingiaji wa mikataba mibovu na usimamizi hafifu wa sheria kutokana na kusababisha ajira nyingi za Watanzania kupotea.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi - Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi alisema kwa sasa Katiba ya mwaka 1977 inaeleza namna ya mfumo na uendeshaji wa serikali na inatambua kuwapo ajira zinazopatikana kwa ushindani na uteuzi.

Alisema serikali kupitia vyombo vyake imekuwa ikichukua hatua katika kuimarisha vyombo vinavyosimamia sheria ikiwamo mahakama, polisi, TAKUKURU na kuchukua hatua kwa wanaoingiza serikali kwenye mikataba mibovu.

"Serikali ina mahakama maalum ya kuchukua hatua kwenye makosa ya kiuchumi na moja wapo ni kudhibiti mambo haya," alisema.

Katika swali la msingi, Mpina alihoji ni vijana wangapi hawana ajira nchini na serikali imewaandaaje kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi wa mwaka 2021 unaonyesha vijana wenye umri wa miaka 15-35 ambao wana ukosefu wa ajira ni 1,732,509.

"Idadi hiyo ni sawa na asilimia 12.2 ya nguvu kazi ya vijana 14,219,191 wenye uwezo wa kufanya kazi kwa maana ya vijana walio katika umri huo na hawapo katika mafunzo au hawana ulemavu unaosababisha wasijishughulishe na shughuli za kiuchumi," alisema.

Katambi alisema katika kuhakikisha vijana wanaandaliwa ipasavyo kushindana katika soko la ajira la ndani na nje, serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Kukuza Ujuzi wa Miaka 10 (2016/2017–2025/2026).

Alisema kupitia mkakati huo, serikali imefanya maboresho ya miundombinu na mitaala katika ngazi za Elimu ya Juu, Elimu ya Kati na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

"Sambamba na maboresho hayo, serikali inatoa mafunzo ya kuwezesha vijana walio nje ya mfumo rasmi wa mafunzo ili kumudu ushindani katika soko la ajira yakiwamo mafunzo ya uanagenzi," alisema.

Pia alisema yanatolewa mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu, mafunzo ya urasimishaji ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo na mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa kutumia teknolojia ya vitalu nyumba.

HABARI KITAIFA

## Majaliwa: PEPFAR imepunguza maambukizi mapya VVU nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Tanzania imefanikiwa kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa asilimia 58 kutoka 130,000 mwaka 2003 hadi 54,000 mwaka 2021 kupitia Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR).

Amesema mfuko huo ambao umeleta mabadiliko makubwa katika mapambano dhidi VVU, pia umesaidia kupunguza vifo kwa asilimia 76 kutoka 120,000 mwaka 2003 hadi 29,000 mwaka 2021.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 20 ya mafanikio katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI yaliyowezeshwa na PEPFAR jijini Dar es Salaam.

Majaliwa alisema Serikali ya Tanzania itaendelea kuunga mkono mpango huo katika kujenga miundombinu ya afya, kutoa mafunzo, kutoa vifaa vya uchunguzi na vifaa vya kinga binafsi, na kuanzisha mifumo ya kufuatilia maambukizi.

"Serikali ya Tanzania inafahamu kwamba Serikali ya Marekani ni mshirika mkubwa katika kukabiliana na VVU nchini, ikiwa imewekeza zaidi ya dola za Marekani bilioni 6.6 kwa ajili ya kukabiliana na janga hilo," alisema.

Majaliwa alisema PEPFAR kwa sasa inasaidia zaidi ya watu milioni 1.5 wanaoishi na VVU (WAVIU) kwenye matibabu kupitia mpango wa kuokoa maisha wa ARV ambapo kabla ya kuanzishwa kwa mpango huo, WAVIU wasiozidi 1,000 ndio walikuwa kwenye Tiba ya Kupambana na VVU.

Alisema Serikali ya Tanzania inajivunia kushirikiana na Serikali ya Marekani kupitia PEPFAR kufikia malengo ya 95/95/95 ifikapo mwaka 2025.

"Hivi sasa kupitia mpango wa PEPFAR tunatekeleza utafiti wa athari za VVU Tanzania kwa mwaka 2022-2023 ambao unakusudiwa kutoa taarifa muhimu katika kuandaa mikakati ya kuzuia maambukizi mapya na kuhakikisha watu wanajua hali zao za VVU," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa PEPFAR Tanzania, Jessica Greene alisema licha ya mafanikio yaliyopatikana, bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma unaongezwa kwa wasichana, wanawake vijana, watoto na makundi ya jamii yaliyo katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa VVU.

Tangu kuanzishwa kwa PEPFAR mwaka 2003, chini ya utawala wa Rais George Bush, Serikali ya Marekani imewekeza zaidi ya dola za Marekani bilioni 100 katika kupambana na VVU/UKIMWI duniani kote, ikijumuisha takriban dola bilioni saba zilizotolewa Tanzania.

## Maelfu wenye vyeti feki walipwa mafao

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako ameupongeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kwa kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kulipa wastaafu mafao kwa wakati.

Vilevile, waziri huyo amebainisha kuwa kati ya watumishi 14,000 waliondolewa kwenye utumishi kwa sababu ya vyeti feki, 6,892 wameshalipwa na 3,169 madai yao yanafanyiwa kazi.

Prof. Ndalichako alitoa pongezi hizo jana mjini Morogoro alipozindua baraza la pili la wafanyakazi wa mfuko huo.

"Mlitumie baraza hili kuhimiza kila mfanyakazi ajue wajibu wake ili kuuwezesha mfuko kusonga mbele katika kutekeleza maagizo ya serikali pamoja na kutoa huduma bora kwa wanachama," aliagiza.

Alisema Rais Samia ameendelea kushughulikia changamoto za wastaafu ikiwa ni pamoja na kuwataka watendaji wa mifuko ya hifadhi ya jamii kulipa mafao watumishi walioondolewa kazini kwa kubainika kuwa na vyeti feki.

"Kulikuwa na jumla ya watumishi 14,000 ambao waliondolewa kwenye utumishi kwa sababu ya vyeti feki, tayari watumishi 6,892 wameshalipwa na 3,169 bado madai yao yanafanyiwa kazi," alifafanua.

Awali Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba alisema kwa sasa mafao hayo ya wastaafu yanalipwa ndani ya siku 60 na uhakiki wa wastaafu unafanyika kidigitali.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya mfuko kwa nusu mwaka toka Julai 2022 hadi Desemba 2022, Kashimba alimpongeza Rais Samia kwa jitihada kubwa alizofanya kuhakikisha Watanzania wengi wanapata ajira.

"Tumevuka lengo la kuandikisha wanachama kwa asilimia 270. Lengo letu lilikuwa kuandikisha wanachama 13,000, lakini tumevuka lengo hilo na kuandikisha wanachama 33,534.

"Sisi wanachama wetu wanategemea jinsi serikali inavyoajiri, watu wengi wameajiriwa katika kipindi hicho," alisema.

Eneo lingine ambalo mfuko umefanya vizuri ni makusanyo ya michango ambapo lengo lilikuwa ni kukusanya Sh. bilioni 792 lakini mfuko umekusanya Sh. bilioni 823 na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 104.

Kuhusu mapato yatokanayo na uwekezaji unaotokana na vitega uchumi, Kashimba alisema mfuko uliweka lengo la kukusanya Sh. bilioni 256 lakini umekusanya Sh. bilioni 297 na hivyo kuvuka lengo kwa kufikia asilimia 116.

Baraza hilo limechagua viongozi wapya wakiwamo Katibu wa Baraza, Steven Biko na Katibu Msaidizi, Linda Njoolay.

## Kinyang'anyiro Askofu Mkuu wa Anglikana chapamba moto

**Na Mwandishi Wetu**

KANISA la Anglikana Tanzania, linatarajiwa kufanya uchaguzi wa Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Februari 9, mwaka huu, jijini Dodoma baada ya mkuu wa sasa, Dk. Maimbo Mndolwa, kumaliza miaka mitano.

Kutokana na kumalizika kwa muda huo, Askofu Mkuu Mndolwa aliyeliongoza kanisa hilo tangu mwaka 2018, anaweza kuchaguliwa kwa miaka mitano kama katiba ya kanisa hilo inavyoainisha.

Askofu Mkuu anaruhusiwa kuongoza kwa vipindi viwili vya miaka mitano kila kimoja na baada ya hapo nafasi yake inachukuliwa na mtu mwingine.

Wakati siku zikisonga kwa ajili ya kutimiza takwa hilo la kikatiba, taarifa za ndani ya kanisa hilo zinabainisha kwamba kumekuwa na kampeni za chini kwa chini ambazo zinawahusu baadhi ya maaskofu kutaka kuingia katika kinyang'anyiro cha nafasi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Mchungaji Bethuel Mlula, alithibitisha kuwa kanisa hilo litafanya uchaguzi wa nafasi ya Askofu Mkuu na kwamba kuna baadhi ya watu wasio na nia njema wamekuwa wakijaribu kuchafua sifa ya viongozi katika mitandao ya kijamii.

"Ni kweli tunafanya uchaguzi mkuu wa kumpata Askofu Mkuu kutokana na Askofu Mkuu Dk. Mndolwa kumaliza awamu ya kwanza ya uongozi wake wa miaka mitano," alisema Mlula.

Alisema pamoja na nia njema ya kanisa ya kumtafuta kiongozi wa juu na kutimiza takwa la kikatiba, kumejitokeza makundi ya watu katika mitandao ya kijamii wakiwachafua viongozi wa Kanisa kwamalengo mabaya.

"Tunapaswa kusali na kumwomba Mungu ili tupate kiongozi atakayeongoza Kanisa letu kwa weledi pamoja na waumini wake," alisema.

Kanisa la Anglikana Tanzania ambalo ni mwanachama wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), ni moja ya makanisa yenye waumini wengi nchini na ina dayosisi 28 nchini.

Pamoja na kwamba Askofu Mkuu anaweza kuongoza kanisa hilo kwa vipindi viwili vya miaka mitano kila kimoja, katika miaka ya karibuni, viongozi wa nafasi hiyo wamekuwa wakiongoza kwa kipindi kimoja na kuondoka. Waliokaa kipindi kimoja katika historia ya kania hilo nchini ni maaskofu wastaafu Dk. Valentino Mokiwa (Dayosisi ya Dar es Salaam) mwaka 2008 hadi 2013 na Dk. Jacob Chimeledya (Mpwapwa) mwaka 2013-2018.

Maaskofu wakuu wengine walioongoza kanisa hilo ni John Sepeku (1970 - 1978), Mussa Kahurananga (1979- 1983), John Ramadhani (1984 - 1998) na Donald Mtetemela (1998 - 2008).




# Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa na mtoto mchanga

**Na Hamisi Nasri,** NANYUMBU

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Chipuputa, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu mkoani Mtwara (jina limehifadhiwa kwa kuwa ni mtoto), ameripoti shuleni akiwa na mtoto mchanga.

Uongozi wa shule umeeleza kuwa mtoto huyo alijifungua baada ya kuhitimu darasa la saba mwezi Oktoba mwaka jana.

Wilayani hapa jana, Mkuu wa shule hiyo, Mwalimu Osmondi Nkanovya alibainisha kuwapo shida hiyo alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu maendeleo ya kuripoti kwa wanafunzi waliochaguliwa kuanza masomo ya kidato cha kwanza mwaka huu.

Mwalimu Nkanovya alisema shule hiyo kwa mwaka huu wa 2023 ilipangiwa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza 194. Kati yao, wavulana ni 93 na wasichana ni 101.

Alisema Shule ya Sekondari Chipuputa imekuwa na mwenendo mzuri wa wanafunzi kuripoti shuleni kwa mwaka huu, akibainisha kuwa hadi jana, walikuwa wameripoti ni 186. Kati yao, wavulana ni 88 na wasichana 98.

Mkuu wa shule alisema kuwa kati ya wanafunzi hao, mmoja aliripoti shuleni akiwa na mtoto mchanga.

"Inaonekana wazi kwamba hata wakati anafanya mtihani wa darasa la saba, wamanafunzi huyo aliufanya akiwa na ujauzito," mwalimu huyo alisema.

Kiongozi huyo wa shule alisema mwanafunzi huyo baada ya kuripoti shuleni na mtoto mchanga, alipokewa kisha kuelezwa kuwa kwa mwaka huu hatoweza kuendelea na masomo ya kidato cha kwanza, hivyo anatakiwa kwenda kumlea mtoto wake na anarejee shuleni mwakani kujiunga na kidato cha kwanza kwa ajili ya kuendelea na masomo yake.

Mwalimu huyo alisema wameshuhudia mwamko mzuri kwa wanafunzi kuripoti shuleni kwa wakati, kukiwa na wanafunzi wanane pekee (akiwamo mwenye mtoto) ambao hawajaripoti shuleni kati ya wanafunzi 194 waliopangwa kuripoti kwenye shule hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu, Mariamu Chaurembo alisema serikali wilayani humo inaendelea kuwafuatilia wazazi na walezi ambao watoto wao hawajaripoti shuleni na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Alisema wapo baadhi ya watoto ambao walipaswa kujiunga na kidato cha kwanza na tayari wamepata ujauzito, hivyo kushindwa kuripoti shuleni na serikali wilayani hapa inaendelea kufuatilia takwimu halisi za wanafunzi ambao wamepata ujauzito ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

# Vijana 147 waliojiunga na JKT wabainika kuwa na VVU

**Na Romana Mallya,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI imesema katika kipindi cha miaka mitatu kilichoanzia 2018, vijana wanaojiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) waliopimwa na kukutwa na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) ni 147.

Ilibainisha hayo jana bungeni ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli zake, taarifa hiyo ilisomwa na mjumbe Yahaya Masare kwa niaba ya mwenyekiti wa kamati.

Masare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, alisema JKT hupokea vijana ambao wamehitimu kidato cha sita ambao huripoti kambini kwa ajili ya mafunzo bila kujali hali ya afya zao, wote hujumuishwa kuhudhuria mafunzo hayo.

"Ingawa kabla ya kuanza mafunzo wote hulazimika kupimwa afya zao, wale ambao watagundulika kuwa wajawazito tu ndio hurejeshwa nyumbani," alifafanua.

Alisema kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2021, JKT ilichukua vijana kwa mujibu wa sheria ambapo mwaka 2019 vijana 20,413; mwaka 2020 vijana 21,383 na mwaka 2021 vijana 25,503. "Hali ya maambukizi kwa vijana waliokuwa kambini kwa mujibu wa sheria kwa miaka hiyo mitatu ni kama ifuatavyo.

"Mwaka 2019 kati ya vijana 20,413 waliopimwa, 60 walikutwa na maambuzi; mwaka 2020 kati ya vijana 21,383 waliopimwa, 45 walikutwa na maambukizi na mwaka 2021 kati ya vijana 25,503 waliopimwa, 42 walikutwa na maambukizi," alibainisha.

Alisema vijana wenye VVU kambini JKT wanapatiwa huduma mbalimbali kama vile ushauri nasaha na kuanzishiwa dawa za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI (ARV).

"Pia hupatiwa vipimo muhimu kabla ya kuanza dawa na hata baada ya kuanza dawa vipimo kama vya figo (Renal function test), maini (Liver function test) na CD4 Count na Viral load (Wingi wa virusi kwenye damu) pamoja na kupimwa magonjwa nyemelezi kama kifua kikuu (TB Screening)," alisema.

Mjumbe huyo pia alisema kuwa pamoja na huduma hizo zinazotolewa na JKT, kamati imebaini kuwa bado elimu kuhusu umuhimu wa kujua afya ni mdogo lakini pia fedha za utekelezaji wa afua hazitoshelezi mahitaji.




Mkuu wa Shule ya St Anne Marie Academy, Gladius Ndyetabura (kulia), akikabidhi zawadi ya vitabu kwa Gladness Peter, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuwa ni miongoni mwa wahitimu 103 wa kidato cha nne wa shule hiyo waliofaulu kwa daraja la kwanza kwenye matokeo yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Chongolo aonya watoto wa kike kugeuzwa kitegauchumi

**Na Mary Geofrey,** MOROGORO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amewataka wazazi na walezi kuacha kugeuza watoto wa kike chanzo cha kuwaingizia kipato na badala yake wawapeleke shuleni.

Pia amepiga marufuku kuwapeleka mijini watoto kufanya kazi za ndani na kuwacheza ngoma wakiwa wadogo kwa kuwa wanashawishika kuingia kwenye uhusiano.

Chongolo alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza nyumbani kwa mjumbe wa shina namba mbili katika Kijiji cha Kiloka wilayani Morogoro Vijijini akiwa katika ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM, miradi ya maendeleo, kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Katika ziara hiyo, Chongolo ameambatana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema na Katibu wa NEC, Issa Gavu.

"Watoto wa kike wapelekwe shuleni siyo chombo cha kuwaingizia mapato. Somesheni watoto wa kike wawe tija kwa familia na taifa.

"Acheni kuwafanya watoto wa kike kuwa watumishi wa kazi za ndani, na wao wanastahili kwenda kusoma na kupata elimu.

"Mwache kuwacheza ngoma, wote tunajua UKIMWI upo, tusiwacheze ngoma, mkawafanya wakaingia kwenye mambo makubwa," alikemea.

Chongolo alisema watoto wote wana fursa sawa ya kupata elimu, ndio sababu serikali imejenga shule za sekondari nchi nzima ili kutoa fursa ya kupata elimu bila malipo kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha sita.

Sambamba na hilo, Chongolo aliwataka wazazi na walezi kuwalea vijana katika maadili yanayofaa.

"Kijana anamaliza darasa la saba, anaanza kujifunza kuendesha bodaboda, wiki moja baadaye anaanza kuendesha. Baada ya miezi miwili anamiliki pikipiki mbili naye anaajiri vijana, wazazi hawahoji wanafurahia tu.

"Msiwashangilie watoto wanaokuja na mafanikio nyumbani, waulizwe maswali wamekujaje na fedha au mali hizo nyumbani?" alihadharisha.

Alisema wazazi wana wajibu wa kuwahoji na kukemea vitendo hivyo ambavyo athari zake ni kubwa kwa jamii na Taifa.

Alipiga marufuku wanawake wajawazito kupelekwa kwa wakunga wa jadi kujifungua, badala ya wapelekwe kwenye vituo vya afya na zahanati zilizojengwa kote nchini.

Awali Katibu wa Shina hilo, Shomari Mkude alimweleza Chongolo kuwa wanakabiliwa na tatizo la udokozi wa mali za wanakijiji.

Alimpongeza kwa kazi kubwa na juhudi zinazofanywa na serikali za kuwapelekea wananchi maendeleo.

# Bil. 17/- zalipwa fidia mradi wa jiji Dar

**Na Beatrice Shayo**

MRATIBU wa mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) Wilaya ya Kinondoni, Mhandisi Mkelewe Tungaraza, amesema zaidi ya Sh. bilioni 17 zimelipwa kama fidia kwa wananchi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Tungaraza alisema hayo juzi wakati wa ziara na waandishi wa habari katika jiji la Dar es Salaam kuangalia utekelezaji wa mradi huo ulioanza mwaka 2016 na kumalizika mwaka jana ambao umegharimu Sh. bilioni 215.9 kwa wilaya ya Kinondoni.

Alisema licha ya mafanikio makubwa yaliyojitokeza katika mradi huo, walikutana na changamoto mbalimbali ambazo zilisababisha mradi kuwa na gharama kubwa.

Tungaraza alisema wakati wa kutekeleza ujenzi kuna maeneo ambayo yalikuwa finyu ikailazimu serikali kulipa fidia ya zaidi ya Sh. bilioni 17 kwa Wilaya ya Kinondoni ili wananchi wapishe mradi.

"Tumewalipa hizo fedha ili tuweke miundombinu ya ujenzi. Unaweza kuangalia hii fedha tungeiweka katika miundombinu tungeongeza kilometa kadhaa za barabara na kutatua changamoto ya usafiri ndani ya jiji.

"Kwenye maeneo ambayo ni njia za maji tulikutana na malalamiko ya wananchi kudai nyumba zao zimechukuliwa na maji. Tunataka kutekeleza mradi mwananchi anadai nyumba yake na kutaka kulipwa fidia wakati sisi nyumba hatujaikuta,"alisema.

Alisema changamoto hiyo imejitokeza kwenye mradi wa Mto Sinza ambao baadhi ya nyumba zimeondolewa na mafuriko kabla ya utekelezaji wa mradi.

Kwa mujibu wa Tungaraza, maeneo hayo yalishazuiwa kwa wananchi kufanya ujenzi, hivyo wamefanikiwa kupambana na changamoto hizo kwa kutengeneza mifereji ili kuokoa nyumba ambazo zipo zisiendelee kupata athari.

Tungaraza alisema katika maeneo yaliyopimwa ya hifadhi ya barabara, wananchi wamejenga nyumba, hivyo kusababisha kuchelewa utekelezaji wa mradi.

Pia alisema kucheleweshwa kulisababishwa kulazimika kufufua mipaka ya viwanja vya wavamizi ili kutambua wameingia kwa kiasi gani na kuwekwa kwa alama na kuzibomoa.

Aidha, alisema mradi wa DMDP umekuwa suluhisho katika kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zinawakabili wananchi wa Kinondoni na Dar es Salaam kwa ujumla.

"Hivi sasa katika maeneo ambayo mradi umetekelezwa mwananchi anayetumia barabara anaweza kutumia njia mbalimbali kutoka eneo moja kwenda jingine bila kukutana na changamoto ikilinganishwa na awali kabla ya mradi kuanza," alisema.

Alisema mradi ulihusisha ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami na zege, usimikaji wa taa za barabarani, ujenzi wa njia za watembea kwa miguu, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua, ujenzi wa vyuo vya umma, ujenzi wa masoko na sehemu za kupumzika.

Tungaraza alisema kwa kiwango kikubwa kero ya mafuriko imepungua hasa katika maeneo ya Mwanayamala, Bwawani, Tandale, Sinza, Kilongawima na Mbweni.

Alisema lengo kuu la DMDP ni kuiwezesha serikali kutoa huduma bora kwa wananchi na kuibua fursa muhimu za uwekezaji ambazo hazijatumika ili kuboresha ukuaji na ustawi wa Jiji la Dar es Salaam katika kukuza uchumi wa nchi na kukabiliana na majanga mbalimbali na mabadiliko ya tabianchi.



Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Martin Shillaa mbaye ni Mratibu wa Mpango wa Usalama Wetu Kata ya Polisi Kariakoo na Kati, akizungumza na baadhi ya wazazi wa watoto wanaosoma Shule ya Msingi Olympio, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, kuhusu kuwa makini kwenye malezi hasa kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha yanayochochewa na utandawazi. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Kampeni SBL kuwainua vijana kimaisha

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Pilsner Lager, imetenga Sh. milioni 36 kwa washindi 22 wa kampeni yake ijulikanayo kama "Kapu la Wana".

Mbali na fedha, washindi pia watajishindia zawadi mbalimbali zikiwamo gari, bodaboda, luninga na simu za mkononi.

Kampeni hiyo inayodumisha kaulimbiu ya chapa yake "SIMAMA IMARA, SONGA MBELE" inarudi kwa mara ya pili ikiwa na dhamira ya kuwapa vijana nafasi ya kujipatia fursa mbalimbali zitakazowasaidia kujikwamua kimaisha. Akizungumza katika hafla fupi ya uzinduzi wa kampeni hiyo iliyofanyika Dar es Salaam jana, Meneja wa Bia ya Pilsner Lager, Wankyo Marando, alisema: "Tukirudi nyuma kuangalia lengo la bidhaa hii, Pilsner Lager ipo kwa ajili ya kusherehekea mafanikio ya walaji wetu na kuwatunza kwa umaridadi wao kutimiza ndoto zao na kuchapa kazi."

Alisema kampeni ya "Kapu la Wana" ni mwendelezo wa bia ya Pilsner Lager kuwazawadia watu walioonyesha udhubutu, kukabiliana na changamoto katika kujikwamua kimaisha na kufanikisha mafanikio waliyojiwekea.

Kwa mujibu wa Marando, kampeni hiyo inaipa Pilsner Lager jukwaa la kuhodhi nafasi muhimu katika maisha ya vijana wachapakazi, wanaojihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

"Pilsner Lager ni bia ya vijana ambao hawakati tamaa na wenye kiu ya kutimiza mafanikio makubwa. Tunawawezesha vijana na kwa kuwapatia vitendea kazi ili wasonge mbele. Tunawahamasisha watumiaji wote wa Pilsner Lager kuitumia kampeni hii ili kusogeza juhudi zao mbele," alisema.

Alisema kampeni ya "Kapu la Wana" ni ya Watanzania wote walioko ndani ya kanda tatu (Kaskazini, Kusini na Kanda ya Ziwa). Watumiaji wanatakiwa kununua bia ya Pilsner Lager, na kukwangua kadi maalum ili kujiweka katika nafasi ya kushinda.

"Kampeni hii itakwenda kwa muda wa miezi minane mfululizo na itahusisha watu wote waliofanikiwa kuingia katika kinyang'anyiro cha kushindania zawadi, baada ya kutuma nambari maalum na kupokea ujumbe mfupi wa udhibitisho," alisema. Mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Salim Mgufi, aliwataka wanywaji wa bia hiyo kushiriki kwenye promosheni hiyo.

# Huduma za kibingwa MOI kuanza kutolewa Tabora

**Na Mwandishi Wetu,** IGUNGA

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) iko mbioni kusogeza huduma zake za kibingwa kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora na mikoa jirani kwenye Hospitali ya Rufani Nkinga ili kuwaondolea wananchi usumbufu na gharama kubwa kufuata huduma hizo Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface amesema imekuwa azma ya serikali kuhakikisha huduma za kibingwa zinasogezwa karibu na wananchi na kuwaondolea usumbufu wa kuzifuata huduma hizo umbali mrefu.

"Tulipokea wito wa wenzetu wa Hospitali ya Rufani Nkinga kuja kutembelea hospitali yao, kuona miundombinu na vifaa vilivyopo ili tuone namna bora ya kusogeza huduma zetu kwa wakazi wa Mkoa wa Tabora na mikoa jirani.

"Leo (jana) tumetembelea hospitali hii na tumeona mazingira yao, kwa kweli wanafanya kazi kubwa na nzuri na sisi tunawaahidi kusogeza huduma zetu hapa kama ambavyo serikali inaelekeza," alisema kiongozi huyo jana baada ya kuzuru hospitalini huko.

Dk. Boniface alisema kwa sasa serikali kupitia Wizara ya Afya na sekta nyingine ipo kwenye mchakato wa bima ya afya kwa wote ambayo itawapa wananchi uhakika wa matibabu ya kibingwa wakati wote.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani Nkinga, Victor Ntundwe alimshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa MOI Dk. Boniface kwa kuitikia wito na ombi la kufika kwenye Hospitali ya Nkinga ili kuona namna bora ya kuanzisha ushirikiano ili kusogeza huduma za kibingwa za mifupa, ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu kwa wakazi wa Tabora na mikoa jirani.

"Leo (jana) imekuwa siku ya pekee kwetu kwani tumempokea Mkurugenzi Mtendaji wa MOI na timu yake ambao pamoja na mambo mengine wametembelea hospitali yetu ili kuona ni namna gani tunaweza kuanzisha huduma za MOI hapa. Kwa kweli tumefarijika sana na tunaamini matunda ya ziara hii yataonekana siku si nyingi," alisema.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani Nkinga, Dk. Tito Chaula alisema ushirikiano kati ya MOI na Nkinga utaleta tija kwa kuwa kwa kipindi kirefu wananchi wamekuwa wakipata usumbufu wa kufuata huduma mbali na kwa gharama kubwa, hivyo kuanza kwa huduma za MOI kwenye hospitali hiyo kutamaliza changamoto hiyo.

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kuheshimu mikataba, silaha kuvutia wadhamini wengine

**MIAKA** ya nyuma klabu pamoja na vyama vya michezo ikiwamo Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), vilikuwa na kilio cha kukosa wadhamini kwa ajili ya kuendesha mashindano yao mbalimbali.

Kila kukicha viongozi wa klabu pamoja na vyama vya michezo hapa nchini walilazimika 'kuombaomba' au msemo maarufu 'kutembeza bakuli' ili kupata fedha za kuendesha ligi zake pamoja na mashindano mengine waliyoyandaa kwa mujibu wa kalenda zao.

Wakati mwingine timu zilikuwa zinakwama hadi kusafiri kwenda katika vituoni au nje ya nchi kupeperusha bendera ya taifa kutokana na kukosa fedha za kugharamia tiketi na pengine kulipa ada ya ushiriki.

Hali hiyo ilizifanya klabu na vyama hivyo mara kwa mara kuyalilia makampuni na taasisi mbalimbali ili zijitokeze kuwekeza kwenye michezo yao ambayo mwisho wa siku ilitoa wawakilishi wa nchi kwenda kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Lakini katika kipindi cha miaka 10 sasa tumeshuhudia makapuni na taasisi mbalimbali zikijitokeza kuingia mikataba ya kudhamini timu au mashirikisho na kubadili taswira ya michezo yetu kutoka kuonekana ya ridhaa na kuwa ya kulipwa.

Udhamini mnono uliopatikana ulisaidia kuboresha ligi na mashindano mbalimbali, lakini pia ulisaidia kuwavutia na kuzipa klabu uwezo wa kusajili wachezaji wa kigeni ambao walisaidia kuongeza nguvu kwenye vikosi vyao na hatimaye timu za Tanzania kuanza kuogopeka.

Timu pia zilipata nguvu ya kuajiri makocha wa kigeni , lakini pia kufanya uamuzi wa kwenda kuweka kambi ughaibuni ili kufanya maandalizi ya kujiandaa na msimu mpya, timu zimenunua vifaa vya kisasa, zimetekeleza programu zake mbalimbali za kiufundi kutokana na fedha walizopata kutoka kwa wadhamini hao.

Ushindani katika ligi mbalimbali uliongezeka kutokana na zawadi nono ambazo sasa hutolewa lakini pia posho za ushindi wa kila mechi, ziliongeza ushindani ambao mbali za kuzipa timu matokeo chanya, wachezaji wa Kitanzania waliimarika na kutoa mchango mzuri pale walipoitwa kwenye Timu za Taifa. Pamoja na mazuri hayo, inashangaza kuona siku za hivi karibuni klabu zimeanza kuvunja makubaliano na wadhamini wao, pengine kwa kudhamiria au kwa kujiona wao ni 'wakubwa' na kampuni hizo hazitawachukulia hatua.

Katika dunia ya sasa ukiona kiongozi anashiriki kuvunja au kukiuka makubaliano yaliyosainiwa, basi huyo haitakii mema taasisi ambayo anaiongoza, kwa sababu ikumbukwe imewachukua muda mrefu mabosi wa makampuni kuwekeza kwenye michezo kwa sababu ya baadhi ya viongozi kujichukulia maamuzi kwa kutoangalia madhara ya baadaye.

Kwa faida ya maendeleo ya michezo hapa nchini, ni vyema viongozi wa Yanga wakakaa upya na kujadiliana kuhusiana na malalamiko ambayo wamepewa na wadhamini wao wakuu, Kampuni ya Kubashiri Michezo ya SportPesa. Ni wazi vikao vya pamoja vinaweza kulimaliza sakata hili ambalo limeonekana kuchafua 'hali ya hewa' wakati Yanga ikibakiza siku chake kuanza kuiwakilisha nchi na bendera ya klabu yake katika mechi za hatua ya makundi ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Tunaamini Yanga na SportPesa bado wana nafasi ya kukaa pamoja na kulimaliza sakata hili na kuifanya 'ndoa' ambayo waliifunga inayotarajiwa kumalizika ifikapo mwaka 2025, ikaendelea kwa amani.


Kuendelea kukiuka mkataba, kunaweza kuigharimu Yanga kama ambavyo Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), ilivyowahi kujiondoka kudhamini Ligi baada ya viongozi waliokuwa madarakani wakati huo TFF ikiitwa FAT kuongeza idadi ya timu kinyume na makubaliano.

Ikumbukwe SportPesa pia ni wadhamini wa timu nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo ni Namungo FC ya Lindi na Singida Big Stars yenye makazi yake mkoani Singida na vile vile hutoa misaada mbalimbali kwa jamii, kitendo cha kuingia katika 'mzozo' na Yanga kinaweza kuathiri shughuli zake na pengine watakaoumia zaidi wakawa ni wadau wa soka hapa nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Hongera TFF, Ligi Kuu kutikisa Afrika, lakini...

Na Adam Fungamwango

**LIGI** Kuu Tanzania Bara kwa sasa imekuwa gumzo barani Afrika, si tu kwa wachezaji wengi kumiminika kuja kucheza tu, lakini kwa sasa imetajwa ni moja kati ya ligi bora, zenye mvuto na kukamata nafasi ya tano.

Shirikisho la Kimataifa la Historia na Takwimu za Mpira wa Miguu (IFFHS) limeitangaza Ligi Kuu Tanzania Bara ni ya tano kwa ubora barani Afrika na ya 39 duniani kwa mwaka 2022, na imepanda kutoka nafasi 10 Afrika na ya 62 duniani, nafasi iliyokuwapo mwaka uliopita.

Ofisa Mtendaji Mkuu, Almasi Kasongo, ameelezea kwa uchache tu ni kitu gani ambacho kimeonekana kwa shirikisho hilo la kimataifa hadi kuiweka Tanzania kwenye tano bora, ikizipiga kumbo Ligi Kuu Afrika Kusini, Angola, Tunisia, Nigeria na Zambia. "Unapofanya jambo ni lazima ufanye utafiti, wataalamu walikaa na wakaja wa matokeo hayo.

Siri kubwa ya kuwa hapa ni utawala bora, uwazi na weledi, Bodi na Shirikisho tumekuwa tukipigania sana hilo, tangu Rais wa TFF, Wallace Karia, alipoingia madarakani unaweza ukaona ni kwa kiasi gani eneo la utawala bora limezidi kuimarika, unapokuwa na utawala bora ni lazima kutakuwa na uwazi na kukiwa na uwazi basi watu watafanya kazi kwa misingi ya weledi. Ukivichanganya vitu hivyo vitatu, mafanikio yake ndiyo haya tumeanza kuyaona," Kasongo alisema.

Niwapongeze TFF na Bodi ya Ligi kwa usimamizi mzuri na kutengeneza mazingira safi na rafiki kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imesababisha kupaa Afrika, japo bado baadhi ya watu wamekuwa na maswali mengi juu ya ligi hii kuzidi kama zile za Afrika Kusini, Zambia, Angola na Tunisia.

Kwangu binfasi naweza kuainisha vitu ambavyo kwa kiasi kikubwa vinaweza kuwa ndiyo vimesababisha Ligi ya Bongo kupanda.

Kwanza kabisa, ninavyojua wachezaji wengi za Zambia awali walikuwa wakikimbilia Afrika Kusini kucheza soka la kulipwa, kuwepo nchini kwa nyota kama Clatous Chama, Moses Phiri wa Simba, Kennedy Musonda wa Yanga, inaonyesha kuwa ligi ya Tanzania kwa sasa imependa sana.

Zamani wachezaji kama kina Chama na Phiri wangekuwa wako Sauzi tu.

Kumiminika kwa wachezaji kila pande wa Afrika mpaka kwa nchi ambazo Wabongo hawakuwahi kuona kama wanaweza kuja kucheza soka hapa, kunaonyesha jinsi gani ligi imepiga hatua. Kuwepo ia kwa idadi kubwa ya wachezaji wanaoruhusiwa kusajiliwa pia kumesabisha hivyo licha ya kwamba hapo awali baadhi ya wahafidhina walikuwa wakipinga, wakitaka wapunguzwe.

Kwa sasa idadi ni wachezaji 12, na wapo wanaotaka msimu ujao waongezeke hadi 15 ili ligi izidi kupanda juu.

Klabu ya Simba kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa mara tatu, na kusababisha ushiriki wa timu nne, huku msimu huu ikiwa imeingiza timu mbili za Simba na Yanga kwenye hatua za makundi kwenye michuano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika, CAF.

Kwa siku za karibuni Bodi ya Ligi pia imekuwa ikidili na waamuzi ambao walionekana hawafanyi vema kwenye mechi mbalimbali.

Waamuzi wengi wamefungiwa, na hawa ndiyo ambao mashabiki wengi wanadai kusababisha soka la Tanzania kudumaa.

Wapo vijana waliopandishwa ambao kwa sasa wanachezesha vyema sana na yale makosa ya kibinadamu ya waamuzi sasa yanafanywa na wachezaji uwanjani, siyo wao tena. Hapa ndipo TFF na Bodi wanapaswa kushikilia bango. Ni eneo linalotakiwa kuwa endelevu na la kutazamwa, ikiwezekana kuazima hata baadhi ya waamuzi kutoka Zanzibar ambao wameonekana kuchezesha vema Kombe la Mapinduzi, nao waje kuongeza nguvu.

Pia eneo la viwanja pia TFF na Bodi kwa siku za karibuni wameonekana kulivalia njuga. Hili nalo linatakiwa kuwa endelevu kwani haitopendeza tena kuona ligi iliyo tano bora Afrika ikichezwa kwenye viwanja vibovu.

Mbali na hayo, yapo pia maeneo mengine kadhaa ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi kama TFF na Bodi wanahitaji ligi ya hapa nchini izidi kwenda juu na kushangaza wengi Afrika.

HABARI KITAIFA

# Gwajima awaangukia wanaume vita ukeketaji

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wanaume na wavulana kushiriki kikamilifu kupinga mila na desturi zenye madhara ili kutokomeza ukeketaji.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuelekea Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji dhidi ya Wanawake yanayofanyika Februari 6, kila mwaka.

Alisema maadhimisho hayo yanalenga kutokomeza vitendo vya ukeketaji dhidi ya wanawake na kaulimbiu ya mwaka huu ni "Wanaume na Wavulana; Tushiriki Kupinga Mila na Desturi zenye Madhara ili Kutokomeza Ukeketaji".

Waziri Gwajima alisema kaulimbiu hiyo inatambua umuhimu wa wanaume katika kushawishi wanawake na watoto wa kike kutofanyiwa ukeketaji.

"Wanaume inatakiwa kubadilika kwanza ndipo jitihada za kupinga ukeketaji zinaweza kufanikiwa. Takwimu zinaonyesha kuwa ukeketaji nchini bado ni tatizo hali inayotokana na baadhi ya jamii zetu kuendelea kukumbatia mila na desturi zenye madhara na kuwadhalilisha watoto wa kike, alisema.

Gwajima alisema serikali inaendelea na jitihada za kukabiliana na vitendo vya ukeketaji kupitia mipango na mikakati iliyowekwa ikiwemo kutunga na kufanya marekebisho .

"Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1997) inasisitiza usawa na heshima kwa binadamu wote, kutambua na kutathmini utu wa mtu pamoja na kuhakikisha haki mbele ya sheria," alisema.

Pia alitoa wito kwa wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha maadhimisho hayo yanafanyika ngazi zote kwa kuandaa mdahalo wa wadau wanaotekeleza shughuli za kutokomeza ukeketaji nchini pia kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukeketaji kwa njia ya mikutano ya hadhara, vikao na maandamano.

Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mtoto kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Asha Vuai alisema serikali inaendelea na juhudi za kupinga ukeketaji dhidi ya wanawake na watoto hasa katika mikoa iliyoathiriwa na ukatili huo akitaja mikoa inayoongoza nchini. "Mikoa inayoongoza kwa ukeketaji na asilimia kwenye mabano ni Manyara (58), Dodoma (47), Arusha (41), Mara (32), Singida (31) Tanga (14), Iringa (nane), Njombe (7) na Pwani nne," alisema Vuai.



Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza katika mkutano wa siku tatu wa uwekezaji wa nishati ulioandaliwa na Kampuni ya Kimataifa ya Energynet, jijini Dar es Salaam juzi, kwa lengo la kuhamasisha masuala ya uwekezaji hapa nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBS yasema wauza chakula wengi hawana vibali

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limesema watoa huduma wengi wa chakula katika mikusanyiko hawajakaguliwa maeneo yao ya kazi na kupata vibali vya shirika hilo.

Kaimu Meneja wa Tathmini ya Vihatarishi vya Chakula, Dk. Ashura Katunzi, alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya uhamasishaji wa wauzaji wa chakula kwenye mikusanyiko.

Mafunzo hayo pia yaliwashirikisha wasafirishaji wa chakula na wasagaji wa nafaka kuhusu sheria, kanuni na miongozo ya shirika katika kuhakikisha jamii inapata chakula bora na salama.

Dk. Katunzi aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuhakikisha wanakamilisha usajili wa maeneo yao kwa mujibu wa sheria.

"Nimeambiwa kwamba mpaka sasa idadi ya watoa huduma ya chakula katika mikusanyiko, wasafirishaji wa chakula na wasagaji ambao wamekaguliwa si ya kuridhisha ikilinganishwa na idadi ya watoa huduma katika jiji la Dar es Salaam. Hii si dalili nzuri kabisa," alisema.

Aliongeza kuwa azma ya serikali ni kuhakikisha inakuwa na mtandao mkubwa unaoshughulikia udhibiti wa ubora na usalama wa chakula.

"Ndiyo maana mnaona kwenye mafunzo haya maofisa wa halmashauri wameshirikishwa. Mzingatie kwamba chakula salama ni kiungo muhimu katika afya ya jamii na pia ukuaji wa uchumi kupitia biashara ya chakula duniani," alisema.

Akitoa mada kuhusu miongozo ya kuzingatia kwenye uzalishaji wa chakula, Ofisa Viwango wa TBS, Stephanie Kaaya, alisema wakulima wanapaswa kuzingatia mfumo bora wa kilimo na kuzingatia pia mfumo bora wa usindikaji.

Aliwaambia waandaji wa vyakula kwamba wanapaswa pia kuzingatia mfumo bora wa kanuni za afya kuanzia usafi wa vifaa, eneo na wafanyakazi, uhifadhi na uondoaji wa taka.

Alisema kwa wale wanaofungasha chakula wanapaswa kuhakikisha kuna taarifa muhimu kwenye kifungashio kama jina la bidhaa, jina na anuani ya mzalishaji.

Kaaya alisema mzalishaji anapaswa kuhakikisha ameandika nchi ambayo bidhaa inatoka, tarehe iliyotengenezwa, tarehe ya mwisho ya matumizi, namna ya kuhifadhi na ujazo.

"Vitu muhimu vya kuangalia katika vifungashio ni kama vile usafi wa vifaa ili kisiweze kusababisha utachafuzi wa chakula, kuhifadhi chakula vizuri, kiwe imara kulingana na mabadiliko ya hali ya hewa na kisiwe kinahatarisha ubora wa chakula wakati wa matumizi na kiwe kinarahisisha usafirishaji na uhifadhi na kisaidie uhifadhi wa mazingira," alisema

Alisema uzalishaji wa bidhaa yeyote kwa kufuata viwango vilivyowekwa kwa bidhaa husika ni muhimu sana kwa ukuaji wa kibiashara.

"Ni vyema wazalishaji wakazingatia viwango ili kukidhi matarajio ya wateja wao iwe katika soko la ndani au la nje ya nchi na watumie fursa kubwa ya masoko nchini, Afrika Mashariki na nchi nyingine duniani," alisema.

## Serikali yakaribisha sekta binafsi uwekezaji nishati

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imeahidi kushirikiana na sekta binafsi kuiwezesha sekta ya nishati kufikia malengo ya kusambaza umeme na gesi kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma hizo.

Waziri wa Nishati, January Makamba alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa wadau na wawekezaji kwenye sekta ya nishati uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Alisema Tanzania ipo tayari katika uwekezaji wa nishati na hivyo serikali imeamua kuungana na sekta binafsi kwa lengo la kuikuza sekta hiyo.

"Kuna mahitaji makubwa kwenye uzalishaji wa nishati, tupo tayari kushirikiana nao, tumewaeleza mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo kwenye nchi yetu ikiwamo amani, sera nzuri, utulivu, umoja, mazingira mazuri ya kufanyia biashara pamoja na vivutio vilivyopo vitakavyowarahisishia kwenye uwekezaji," alisema January.

Mwenyekiti wa Bodi Jumuiya ya Watoa Huduma Sekta ya Mafuta na Gesi, Abdulsamad Abdulrahim alisema kukutana kwa wadau wa mafuta na gesi katika mkutano huo kutaileteа nchi matokea chanya.

Alisema wawekezaji walijitokeza kwenye mkutano huo wana shauku ya kuona nchi inapiga hatua, akiomba serikali kukaa na kutafakari jinsi ya kutumia fedha za nje katika uwekezaji.

"Tunashawishiana na tunapeana miongozo mbalimbali katika sekta ya nishati, kwenye mazungumzo watu ambao hawakuwahi kuja Tanzania wanasema nchi zao zimepiga hatua kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, na wao wanataka kuiona Tanzania katika hali hiyo.

"Ninataka kuona uamuzi unafanyika. Kama Tanzania inahitaji kufanikiwa katika eneo hilo, lazima viongozi waachane na urasimu, tuwe wakweli, watendaji wa serikali wafanye kazi kwa bidii, waondokane na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea," alishauri.

Simon Gosling, Meneja wa Energy Net Limited ambao pia ni miongoni mwa waandaji wa mkutano huo kutoka Afrika ya Kusini, alisema ipo haja wadau wa sekta ya nishati duniani kuunganisha nguvu ya pamoja ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi hiyo unafanyika kwa ufanisi na kuleta tija kiuchumi.

Mkutano huo unafanyika kwa siku tatu nchini kuanzia juzi.

# Mfuko nishati safi watoa ruzuku bil. 3.2/-

**Na John Badi**

MFUKO wa Nishati Safi ya Kupikia (CookFund) Tanzania umetoa ruzuku yenye thamani ya Sh. bilioni 3.2 kwa kampuni 16 zinazojishughulisha na huduma za uuzaji wa nishati safi ya kupikia nchini.

Lengo la ruzuku hiyo ni kuzisaidia kutoa huduma kwa gharama nafuu na zenye ubora unaowanufaisha wateja wa kipato cha chini nchini.

Fedha hizo ni matokeo ya mwito wa kwanza wa maombi ya ufadhili yaliyotolewa Septemba, mwaka jana kupitia program hiyo inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) ukilenga katika maeneo ya teknolojia safi ya kupikia hususani gesi, majiko ya umeme, ,majiko ya mkaa banifu, mkaa tofali utokanao na vumbi la makaa ya mawe na nishati ya mafuta itokanayo na mabaki ya mimea.

Hafla fupi ya kukabidhi hundi za fedha kwa wanufaika hao ilifanyika juzi jijini Dar es Salaam ikiongozwa na Waziri wa Nishati, January Makamba, na Balozi wa EU Tanzania, Manfredo Fanti. Wengine waliohudhuria hafla hiyo ni Mkuu wa Mfuko wa Maendeleo ya Mitaji wa Umoja wa Mataifa (UNCDF) Tanzania, Peter Malika, ambaye mfuko wake ndio unaratibu program hiyo.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Waziri Makamba aliwasisitiza wanufaika kuhakikisha wanazitumia fedha hizo kulingana na malengo ya mpango ili matokeo mazuri na kuwafikia Watanzania wengi.

"Ni vyema mkafahamu kuwa huu si mkopo bali ni ruzuku ambayo mnaipata moja kwa moja kwa jina la nchi yetu, hivyo ni vyema mkahakikisha Watanzania wananufaika kweli kupitia mpango huu kwa kuwafikishia bidhaa zenu za nishati kwa bei nafuu ili kuondokana na matumizi ya nishati chafu ambazo si rafiki kwa mazingira," alisema.

Akizungumzia zaidi programu ya CookFund, Waziri Makamba alisema ni moja ya suluhu ya msingi kwa nchi katika kupambana na matumizi ya nishati chafu kwa sababu inawahakikishia wananchi upatikanaji wa nishati safi kwa gharama nafuu.

Balozi Fanti aliwataka wafanyabiashara walionufaika na ruzuku hiyo kuonyesha wanaweza kuuza bidhaa zao kwa bei nafuu na kwa wateja wengi wapya kupitia msaada wa kifedha walioupata kupitia mpango huo

"EU inatarajia ruzuku hizi zitasaidia watumiaji wapya wa nishati ya kupikia hapa nchini kupata vifaa vyote vinavyohusika na mfumo mzima wa zana za kupikia kwa bei nafuu na zaidi tuendelee kuhamasisha Watanzania wengi zaidi waendelee kuachana na mbinu za kupikia ambazo zinachafua na kuharibu mazingira.

"Tunatumai kushuhudia matokeo ya kuridhisha katika siku zijazo na kupungua kwa familia zinazotumia nishati ya kuni au mkaa kwa kupikia," alisema.

Naye Malika alisema kwa kuzingatia athari kubwa ya matumizi ya nishati itokanayo na mimea katika suala zima la mapishi, kuna haja ya msingi ya kuongeza uwekezaji katika mnyororo wa thamani kwenye nishati safi ya kupikia ili kuharakisha mabadiliko kuelekea kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Kwa kuwa hii ni awamu ya kwanza ya maombi yaliyoidhinishwa ambayo yanahusisha wanufaika 16 ambao kwa jumla watahudumia kaya 191,336 katika maeneo yao na kutoa ajira 191 katika kipindi cha miaka mitatu, tunatarajia kuzindua mwito mpya wa mapendekezo mwezi huu, hivyo kuendelea na awamu nyingine ya ruzuku kwa kama hii,"alisema.

CookFund ni programu ya miaka mitatu inayofadhiliwa na EU chini ya mpango wa mkakati jumuishi wa kutumia nishati safi ya kupikia nchini na Mfuko wa 11 wa Maendeleo ya Ulaya (EDF), unaolenga kuchangia dhamira ya Tanzania ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuongeza idadi ya watu na upatikanaji endelevu wa ufumbuzi wa kupikia.



Viongozi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, wakichimba msingi juzi, kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa kisasa, ambao ni mmoja ya miradi ya kimkakati ya kukuza uchumi wa chama hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# LHRC waibuka na hoja tatu tume kuboresha haki jinai

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimetoa mapendekezo matatu kwa Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini ili yasaidie katika shughuli za tume hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi kwenye makao makuu ya kituo hicho, Kijitonyama, Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga alisema moja ya mapendekezo hayo kuwa ni tume kutoa ratiba na usikilizaji wa wazi wa maoni ya wananchi.

"Njia hiyo itasaidia wadau mbalimbali kupeleka maoni ya kuboresha mfumo wa haki jinai nchini. Pendekezo hili litasaidia kamati kuja na taarifa yenye wigo mpana wa mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla," alisema Anna. Mkurugenzi huyo alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza malalamiko miongoni mwa wadau, huku akitaja pendekezo la pili ni kupitiwa upya mfumo wa upelelezi kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

"Pendekezo letu la tatu ni tume kuweka kipaumbele cha kuboresha sheria 31 ikiwamo ya kudhibiti dawa za kulevya ya mwaka 2015 na Sheria ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007," alisema. Pia aliitaja Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 1985, Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya Mwaka 2008.

Alisema kituo hicho kinapongeza jitihada za Rais zinazolenga kuboresha mfumo wa hakijinai, na kwamba mara kwa mara amekuwa akitoa kauli chanya zenye nia ya kufanya maboresho katika mfumo huo.

Anna alisema kuwa kutokana na uteuzi huo wa Rais, wameona kuna haja kutoa mapendekezo ambayo wanaaamini yatasaidia kuboresha shughuli za tume hiyo kwa manufaa ya Watanzania.

"LHRC imekuwa mstari wa mbele katika uchechemuzi wa sheria kwa kupendekeza namna bora ya kuboresha mfumo wa haki jinai, ili kulinda haki za binadamu kupitia mifumo na taasisi za haki jinai," alisema.

Pia aligusia ripoti ya kituo hicho ya Haki za Binadamu ya mwaka 2020, kuwa ilibaini kuwapo kasi ndogo upelelezi au uchunguzi, huku watuhumiwa wakiwa mahabusu, pia ubambikaji wa kesi.

Ripoti hiyo ilianisha kwamba mwaka 2020 mahabusu 1,422 waliachiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka baada ya kubainika walikuwa wamebambikwa kesi," alisema.

Alifafanua kuwa kutokana na mazingira hayo, kituo chake kimetoa mapendekezo kwa tume ilioundwa na Rais, lengo likiwa kuhakikisha makosa ambayo hujitokeza kwenye maeneo mbalimbali, hayajirudii.

Januari 6 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan aliteua wajumbe wa tume hiyo itakayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande.

# Waliofanya vizuri sasa kupelekwa Ngorongoro

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa shule ya St Anne Marie Academy waliofanya vizuri kwenye matokeo ya kidato cha nne wanaandaliwa ziara ya kutembelea mbuga za wanyama za Mikumi na Ngorongoro kama motisha ya kuwafanya wengine nao wafanye vizuri.

Mkuu wa Shule hiyo, Gladius Ndyetabura, alisema jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii kuhusu matokeo ya kidato cha nne. Katika mtihani uliofanyika mwaka jana, wanafunzi 103 wa shule hiyo walipata daraja la kwanza.

Alisema kwenye mtihani huo, wanafunzi 40 walipata daraja la pili na wanafunzi saba pekee ndio wamepata daraja la tatu.

"Haya ni matokeo mazuri sana kwetu ukizingatia tulikuwa na wanafunzi wengi lakini wote wamefanikiwa kupata nafasi ya kuendelea na kidato cha tano ndiyo maana tunawaandalia safari hii ya kwenda Mikumi na Ngorongoro kama motisha kwao na kwa wenzao ili wapate ari ya kufanya vizuri," alisema.

Aliwapongeza na kuwashukuru walimu wa shule hiyo ambao wamefanya kazi kubwa usiku na mchana kuhakikisha wanafunzi wote wanafaulu kwa ufaulu wa juu na alimshukuru pia Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Jasson Rweikiza kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa walimu.

Alitaja siri ya mafanikio hayo kuwa ni shule kuwa na mazingira mazuri ya wanafunzi kusomea ikiwemo maktaba ya kisasa na maabara iliyosheheni vifaa vya kutosha pamoja na walimu mahiri wanaojua kazi yao "Wanafunzi wetu wanakula milo minne kwa siku na tuna mashamba ya mboga mboga na matunda kwa hiyo wanakula mlo kamili na mazingira kwa ujumla ni mazuri sana kuwawezesha kujisomea muda wowote," alisema

Alisema shule hiyo imedhibiti ulinzi kwa kuweka walinzi 46 wenye mafunzo wakisaidiwa na mbwa wao ambao wamekuwa wakizunguka usiku na mchana kuhakikisha kunakuwa na usalama.

"Hawa walinzi wetu wamepata mafunzo ya kisasa kiasi kwamba hata ukitokea moto wakotayari kuuzima ndani ya dakika chache kwa hiyo wazazi msiwe na wasiwasi kuhusu taaluma na suala la usalama," alisema.

Mwaka 2021 St Anne Marie Academy ilitoa mwanafunzi bora kitaifa, Elulei Haule anayesoma kidato cha kwanza shule ya Marian Boys ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani.

Akizungumza kwenye mahafali ya kidato cha nne jana, Dk. Rweikiza, alitangaza kwamba hakuna mwanafunzi yoyote wa shule hiyo atakayefukuzwa kwa sababu ya kufiwa na wazazi wake na kukosa ada.





# Ukata watajwa kikwazo utekelezaji wa MMMAM

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM) mkoani Dodoma imekutana na kutoa tathmini ya robo ya mwaka, ikibaini kuwa moja ya vikwazo vya utelelezaji wa masuala hayo ni ukosefu wa fedha.

Kutokana na hali hiyo kikao hicho kimeazimia kwenda kuhamasisha ili bajeti ya utekelezaji wa MMMAM iingizwe kwenye mipango ya halmashauri.

Akizungumza jijini Dodoma jana, Ofisa Maendeleo ya Vijana Mkuu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Tumaini Masamale alisema ukosefu wa fedha umeonekana ni moja ya kero zinazokwamisha utekelezaji wa masuala ya MMMAM.

"Zipo changamoto kadhaa kwenye utekelezaji wa mpango hususani za kibajeti na upatikanaji wa taarifa. Hata hivyo, katika kikao hiki tumezipitia na kuweka mkakati wa pamoja wa kuzitatua ikiwa ni pamoja na halmashauri kuupa umuhimu mpango huo kwa kuuingiza kwenye bajeti zao ili kuwezesha utekelezaji wake kote nchini," alisema Masamale.

Vilevile, alisema kikao hicho pia kimeazimia kuimarisha uhusiano na wadau wanaotekeleza mpango huu ili wafanye kazi kwa karibu na kuwezesha upatikanaji wa taarifa na kuendelea kushirikisha wadau wengi zaidi wakiwamo viongozi wa dini ili kupanua wigo wa kufikisha ujumbe wa MMMAM kwa jamii.

Mkaguzi wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto Polisi Mkoa wa Dodoma, Yasinta Kayombo alisema bado kuna tatizo kwenye malezi na makuzi ya watoto linalosababishwa na utandawazi.

Aliwataka wazazi kukagua na kufuatilia katuni, tamthilia na nyimbo wanazoangalia watoto kwenye televisheni au kwenye simu za kiganjani kwa kuwa zimekuwa moja ya vitu vinavyochangia kuharibu malezi na makuzi ya watoto.

"Wakati serikali inapambana kuhakikisha kunakuwa na malezo mema kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8, bado kuna changamoto hasa zinazotokana na utandawazi, watoto wamekuwa wakitumia simu za kiganjani za wazazi wao au televisheni kuangalia katuni, tamthilia na hadithi mbalimbali.

"Mwisho wa siku katikati ya katuni hizo au tamthilia na nyimbo kumekuwa na maneno ama vitendo ambavyo havina maadili ambavyo watoto hawa ambao ni wadogo, wanajifunza na kushika haraka sana na hivyo kuchochea vitendo vya ukatili baina ya watoto kwa watoto na hivyo kuathiri Malezi na makuzi yao kwa namna moja ama nyingine," alisema Kayombo. Ofisa Maendeleo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Madlina Kalinganira alisema wanaendelea kutekeleza PJT-MMMAM kwa kushirikiana na wadau husuan wanaotekeleza afua za watoto wilayani humo kwa lengo la kufikisha elimu ya MMMAM kwa jamii.

# Serikali yatoa siku saba za kudhibiti kelele, mitetemo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo ametoa siku saba kwa maeneo yote ya nyumba za ibada na kumbi za starehe yanayofanya uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo, kujirekebisha katika utoaji wa huduma zao ili ziendane na matakwa ya sheria ya mazingira na kanuni zake.

Dk. Jafo alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na kelele na mitetemo.

Aliliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kufungia maneneo yote yatakayokaidi kutekeleza sheria na kanuzi za mazingira kuhusu kelele na mitetemo.

"Kila mwananchi ahakikishe anapofanya shughuli zake hasababishi kelele zinazozidi viwango vinavyokubalika, wamiliki wa nyumba za ibada na kumbi za starehe wahakikishe sauti zitokanazo na shughuli zao hazizidi viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria.

"Wamiliki wa maeneo ya burudani, starehe na nyumba za ibada wazingatie matumizi ya vipima kelele na vizuia sauti ili kuhakikisha jamii zinazozunguka maeneo hayo haziathiriwi na kelele wanazozisababisha," alisema.

Vilevile, aliwataka wananchi kutoa taarifa kuhusu kelele na mitetemo kwenye ofisi za serikali za mitaa au ofisi za Baraza la Taifa la Mazingira.

Pia aliwataka wananchi kuhakikisha kelele na mitetemo zinakuwa ajenda ya kudumu katika vikao vya wakazi ili kulipatia ufumbuzi suala hilo.

"Vilevile, nichukue fursa hii kuzitaka wizara za kisekta, taasisi za umma, sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha zinatekeleza majukumu yao yaliyoainishwa kwenye mwongozo wa udhibiti wa uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele na mitetemo wa mwaka 2021," alisema.

Alielekeza NEMC kwenye kanda zote kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa kanuni za udhibiti wa kelele na mitetemo za mwaka 2015, hasa kwa kuhakikisha wazalishaji sugu wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele na mitetemo wanachukuliwa hatua kali ikiwamo kufungiwa shughuli zao. Dk. Jafo alisema hatua za kisheria zilizoainishwa kwenye sheria ni pamoja na kutozwa faini na kufungiwa biashara kwenye maeneo yaliyokithiri kwa kelele na mitetemo.

Alisema pamoja na kuchukua hatua hizo za kisheria, kumekuwa na ongezeko la malalamiko ya kelele na mitetemo.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 asilimia 65 ya malalamiko yaliyowasilishwa Baraza la Mazingira yanahusu kelele na mitetemo, hali inayoonyesha adhabu za kutozwa faini kwa wanaokamatwa zimezoeleka na hazitoshi.

Waziri Jafo aliyataja maeneo ya starehe zaidi ya 25 kwenye mikoa mbalimbali ya nchi ambayo yamekuwa kinara wa kukiuka sheria na kanuni za mazingira kwa kufanya shughuli zao kwa kelele na mitetemo.



Wanafunzi walioiwakilisha Tanzania nchini Uswisi na kushika nafasi ya pili kwenye mashindano ya "First global robotics challenge", wakiwa wamesimama wakati wakitambulishwa Bungeni, jijini Dodoma juzi. Wanafunzi hao waliohudhuria mafunzo ya kuunda roboti kuanzia Machi 2022 kupitia taasisi ya Apps and Girls, inayofadhiliwa na Tigo, wamealikwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (hayupo pichani), kwa ajili ya kuonyesha ubunifu wao kwa wabunge. Shindano la mwaka jana lilibeba maudhui ya kulinda hali ya hewa ya dunia kwa kuunda mashine(roboti) itakayosaidia kupunguza hewa ya ukaa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yataka wanaume washirikishwe ukeketaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema ukeketaji nchini bado ni tatizo, hali inayosababishwa na baadhi ya jamii kuendelea kukumbatia mila na desturi zenye madhara na kuwadhalilisha watoto wa kike.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima aliyasema hayo jana alipozungumzia Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji dhidi ya Wanawake na Watoto Duniani ambayo hufanyika kila mwaka ifikapo Februari 6.

Alitaja madhara hayo ni pamoja na kupoteza damu nyingi na kusababisha vifo, maambukizi ya VVU/UKIMWI na kusababisha matatizo wakati wa kujifungua.

"Watoto wakati wa kukeketwa hushindwa kuhudhuria shule kwenye vipindi kwa muda mrefu na hivyo kuzorotesha maendeleo yao kielimu," alisema.

Dk. Dorothy alisema serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea na jitihada za kukabiliana na vitendo vya ukeketaji kupitia mipango na mikakati iliyowekwa ikiwamo kutunga na kufanya marekebisho ya sheria na sera mbalimbali za nchi.

Alifafanua kuwa maadhimisho hayo yanalenga kuhamasisha jamii kukomesha vitendo vya ukeketaji kwa wanawake na watoto na kuwashirikisha wanaume na wavulana kushiriki kupinga mila na desturi zenye madhara ili kutokomeza ukeketaji.

"Hivyo, kupitia maadhimisho haya wanaume na wavulana wanaweza kujipima na kukataa ukeketaji kwa wanawake na watoto wa kike na kuona ni kwa namna gani wanaweza kusaidia kupunguza na kukabiliana na vitendo hivyo na kutatua changamoto zinazojitokeza katika mapambano haya na kubuni mikakati mipya," alisema.

Aliongeza kuwa kuna umuhimu wa wanaume na wavulana katika kushawishi wanawake na watoto wa kike kutotamani kufanyiwa ukeketaji.

"Kwa ajili hiyo, mitazamo ya wanaume inatakiwa kubadilika kwanza ndipo jitihada za kupinga ukeketaji zinaweza kufanikiwa," alisema.

Alitoa wito kwa wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha maadhimisho hayo yanafanyika ngazi zote kwa kuandaa mdahalo wa wadau wanaotekeleza shughuli za kutokomeza ukeketaji nchini, pia kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya ukeketaji kwa njia ya mikutano ya hadhara, vikao na maandamano.





# CCM yashtukia ucheleweshaji ushushaji mchele bandarini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU wa Idara ya Itikadi na Uenezi ya Chama Cha Mapinduzi ya Kamati Maalum ya NEC, Khamis Mbeto Khamis ameutaka uongozi wa Shirika la Bandari la Zanzibar kuhakikisha meli zote zenye shehena ya mizigo ya chakula, ikiwamo mchele zinapewa kipaumbele kushusha bidhaa hizo.

Mbeto alisema hayo alipozuru kwenye Bandari ya Malindi, Unguja kuangalia shughuli za kushusha bidhaa mbalimbali za chakula.

Alisema meli zote za bidhaa za chakula, ikiwamo mchele, zinapaswa kupewa kipaumbele zinashusha bidhaa hizo kwa ajili ya kusambazwa kwa wafanyabiashara.

Alisema katika kipindi cha mwezi mmoja, bei ya mchele imepanda hadi kufikiya Sh. 3,000 kutoka Sh. 1,700 kwa kilo, kitendo ambacho kimeibua manung'uniko mengi kwa jamii.

Alisema chanzo kikubwa cha kupanda kwa bei hizo kwa mujibu wa wafanyabiashara ni kukosa nafasi ya kushusha bidhaa za chakula kwa wakati kutoka kwenye meli. "Ninauagiza uongozi wa Shirika la Bandari la Zanzibar kuhakikisha kuanzia sasa meli zilizobeba shehena ya bidhaa za chakula ikiwamo mchele, zipewe kipaumbele kufunga gati na kushusha bidhaa hizo," aliagiza.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Mustafa Kitwana alisema wamejipanga kuhakikisha wafanyabiashara wote wanaosambaza bidhaa za vyakula kuona kwamba zinawafikia walaji katika bei iliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema mfanyabiashara ambaye atajipandisha bei yake kwa maslahi yake pamoja na tamaa ya kupata kipato kikubwa, atachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kunyang'anywa leseni ya biashara.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari Zanzibar, Nahaat Mohamed Mahfoudh alisema changamoto kubwa inayolikabili shirika kwa sasa ni ufinyu wa eneo la meli kufunga gati na kushusha bidhaa zikiwamo za vyakula.

Alisema wameanza kuyafanyia kazi maagizo ya viongozi mbalimbali wa serikali na chama kuona bidhaa za vyakula zinapewa kipaumbele na kushushwa kwenye Bandari ya Malindi kwa wakati.



Wananchi wakiangalia gari la mizigo lilobeba mchanga likiwa limepinduka baada ya kufeli breki katika barabara ya Bububu kwa nyanya, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Marufuku kuingiza ndizi, migomba visiwani Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo imekumbusha uamuzi wake wa tangu mwaka 2017 wa kupiga marufuku kufanya biashara ya ndizi au kuingiza visiwani humo ndizi na migomba kutoka nje ya Zanzibar ili kudhibiti maradhi ya migomba kusinyaa.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio la kuonekana kwa mfanyabiashara wa kike aliyetajwa kwa jina moja la Veronika aliyeingiza ndizi toka Tanzania Bara kupitia Bandari ya Malindi, Waziri wake, Shamata Shaame Khamis alisema ni kosa kisheria kuingiza ndizi Zanzibar kutoka nje ya visiwa hivyo.

Alisema adhabu kwa atakayekamatwa kuingiza ndizi au mgomba Zanzibar ni kifungo cha miezi sita au faini ya Sh. 50,000 au adhabu zote mbili.

Alisema Januari 31 mwaka huu, majira ya asubuhi, maofisa wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwenye kituo cha ukaguzi wa mazao Bandari ya Malindi, walikamata masanduku 15 ya nyanya yaliyotumika kubeba ndizi ambazo hazikuwa na kibali cha kuingiza Zanzibar, pia kukiuka zuio hilo.

"Karantini iliyowekwa chini ya Sheria ya Hifadhi ya Mimea Na. 9 ya Mwaka 1997 bado ipo. Karantini hii iliwekwa mara ya kwanza mwaka 2007 na kurejewa tena mwaka 2017, bado karantini hii inaendelea hadi hivi tunavyoongea," alisema.

Waziri huyo alisema mama huyo aliyekamatwa, alitakiwa kulipa faini ya Sh. 50,000 na kutakiwa ndizi hizo kuzirejesha alikozitoa lakini ndizi amezitelekeza bandarini hapo baada ya kulipa faini hiyo.

Alisema karantini (zuio) ya kuingiza mazao ya migomba na ndizi inatokana na kuibuka kwa maradhi ya mnyauko (bacterial wilt) yanayoathiri zao la migomba kwa ujumla.

Alisema karantini hiyo imefanywa kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi ya Mimea Na. 9 ya Mwaka 1997 katika jedwali la pili ambalo limeorodhesha migomba na mazao yake kuwa ni miongoni mwa mazao yaliyozuiwa kuingizwa Zanzibar.

Alisema maradhi hayo hayapo nchini kwa sasa, ila husababisha hasara kubwa kwa wakulima hadi kufikia upotevu wa asilimia 90 ya mazao kwenye maeneo yanayoathirika na maradhi hayo.

Alisema zuio hilo pia lilifanywa kwa kuwa ni vigumu kuhakikisha migomba na mazao yake yanayoingizwa nchini hayana visumbufu vya maradhi (bacteria na fungus) vinavyoathiri migomba.

"Zanzibar ina aina zisizopungua 30 za migomba, baadhi zinapatikana zaidi kwenye visiwa vyetu ukiwamo mgomba pori maarufu ambao unapatikana kwenye hifadhi zetu za taifa.

"Zuio hili lina lengo la kuilinda Zanzibar na migomba yetu, ikiwamo ile ambayo hailimwi kwa wingi kwenye nchi nyingine," alisema.

Aliongeza kuwa agizo la zuio hilo lilitolewa kwa mara ya kwanza na wizara yenye dhamana ya kilimo mwaka 2007, kwa kutoa tangazo la kutoingiza mazao ya migomba Zanzibar kutokana na kuzuka kwa maradhi ya mnyauko.

Alisema kuwa katika mwaka 2020 kulizuka maradhi mapya yanayojulikana kama Fusarium wilt (TR4) yanayosababishwa na fangasi.

Alisema maradhi hayo yameonekana kushambulia zaidi kwenye maeneo yaliyoshambuliwa na maradhi ya mnyauko katika nchi jirani za Uganda na Tanzania Bara hasa kwenye maeneo ya ukanda wa maziwa makuu.

"Kagera ikiwa ndio waathirika wakubwa nchini, maradhi ya Fusarum Wilt - TR4 yameripotiwa kuwapo nchini Msumbiji na kusababisha hasara ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 30 kwenye mashamba makubwa ya migomba," alisema.

Aliongeza kuwa maradhi hayo ni hatari na yanaweza kusababisha hasara kubwa ya kupungua kwa mavuno ya ndizi kutokana na kufa kwa migomba mingi kwa kipindi kifupi.

Alisema Zanzibar inajitosheleza kwa zao hilo na haihitaji ndizi za Tanzania Bara, ndiyo maana inakataza uingizaji wa ndizi za ziada.

# Rais: Serikali inatambua mchango taasisi za dini

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema taasisi za dini zina mchango mkubwa kwa serikali, hasa katika jukumu zima la kuendeleza amani Zanzibar.

Amesema taasisi hizo ndizo zinazowalea vijana kiimani, weledi, ujasiri na uzalendo kwa taifa na viongozi wao, jambo ambalo linaimarisha amani na uthubutu wa kufikia maendeleo.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar alipozungumza na uongozi wa Jumuiya ya Sunni Jamaat waliofika kujitambulisha jana.

Alisema taasisi binafsi na za kidini zina jukumu la kuisaidia serikali kuendeleza huduma za jamii, akishukuru jumuiya hiyo kwa juhudi za kuendeleza elimu Zanzibar.

Alizitaka jumuiya za dini kuendelea kuishauri serikali kwa mawazo yatakayojenga na kuleta ufanisi kwenye misingi ya maendeleo ya taifa. Dk. Mwinyi pia alizungumzia changamoto zinazoikabili sekta ya elimu, ukiwamo uhaba wa vifaa vya maabara, maktaba, madawati, kompyuta na vitabu.

Alisema serikali imejenga shule 48. Kati yake, 10 za ghorofa kwa lengo la kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

"Kwa hatua tuliyofikia, matokeo yanaweza yasionekane leo, maana ukianza kuigeuza elimu faida yake itaonekana miaka mingi baadaye," alisema Rais Dk. Mwinyi.

Alisema serikali pia inafanya utafiti wa kina kutafuta suluhu ya wanafunzi wengi kufeli na kuweka mikakati imara itakayoinua sekta ya elimu, Zanzibar.

"Safari hii tumeamua kufanya utafiti maana changamoto za elimu ni nyingi mno kila kona huwezi kuziepuka, kuanzia idadi ya wanafunzi kwenye madarasa, ndio maana tunajenga skuli mpya ili kupunguza idadi ya wanafunzi wengi darasani," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali pia inaangalia upya mfumo wa elimu ambao wanafunzi wengi huanza msingi lakini wanapoingia vyuoni, wachache hupata nafasi hiyo, hivyo kuwa na kundi kubwa linalofeli.

Wanajumuiya hao walimshukuru Dk. Mwinyi kwa juhudi za serikali yake kwenye kuiinua sekta ya elimu nchini na kubainisha kuwa wameshuhudia mafanikio makubwa ndani ya miaka miwili ya uongozi wake hasa kwenye kutoa kipaumbele kuimarisha huduma za jamii.



**AMBER ROSE**

UKURASA 14

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI FEBRUARI 4, 2023



# HUYU HAPA HUYU!

NANI kasaini kuwa msanii mpya katika lebo ya WCB? Swali hilo limebaki bila majibu, lakini baadhi ya watu wameanza kubashiri ni nani aliyekula dili hilo nono.

Hata hivyo jina la Mavokali, limekuwa likitajwa sana kuwa ndiye aliyeanguka saini kuingia katika lebo hiyo inayoongozwa na Diamond Platnumz.

Juzi lebo ya WCB ilitangaza kumsainisha mwimbaji nyota wa kizazi kipya.

Watu wanamuhusisha Mavokali na tukio hilo, kutokana na yeye mwenyewe kuandika muda mfupi siku hiyo hiyo kuwa amekamilisha dili.

Kama vile haitoshi, Mavokali amefuta picha zake zote katika mtandao wa Instagram, kama ishara ya kuanza ukurasa mpya wa maisha yake.

Hata hivyo, Diamond mwenyewe wala uongozi wa lebo ya WCB hakuna aliyejitokeza kuthibitisha.

Kama ni kweli Mavokali ameiingia rasmi WCB, basi ataungana na wasanii wengine ambao wapowapo kwa sana Wasafi, ambao ni Mbosso, Zuchu, Lavalava na Queen Darleen.

BASI SAWA

## Idris Sultan akimbiza Netflix

MUIGIZAJI na muandaaji wa filamu nchini, Idris Sultan ameingia tena kwenye soko la filamu la kimataifa baada ya kushiriki 'Married To Work' kazi ambayo inatarajiwa kuuzwa Netflix.



Filamu hiyo itatambulishwa Februari 10 Mwaka huu, kupitia mtandao wa Netflix, imechezwa na wasanii kutoka nchi tatu ambazo ni Tanzania, Kenya na Nigeria.

Akizungumza na NIPASHE jana Idris Sultani, amesema soko la filamu za kiswahili linakua kwa kasi kutokana na juhudi zinazofanywa na wasanii pamoja na waandaaji wazawa kutoka nchini.

"Ubunifu wetu kwenye sanaa unakua siku hadi siku, kama Taifa, hatua hii inatufungulia masoko ya kimataifa na majukwaa makubwa ya filamu, tunafanya watu watufuatilie" amesema Sultan.

## Happy Sanga kuimba kimombo zaidi

Mwimbaji anayefanya vizuri kutoka jijini Mbeya, Happy Sanga, amewaweka tayari mashabiki zake kupokea nyimbo mfululizo za lugha ya Kingereza.

Happy Sanga anayetambulika kama sauti ya upako, ameliambia BT kuwa ameamua kutumia njia hiyo ili kuwafikia mashabiki walio nje ya Tanzania ambao Kiswahili kinawapa tabu.

"Mwaka jana nilikuwa Zambia kwenye mji wa Kapilimposhi , kule watu wengi hawaelewi kiswahili kwa hiyo muziki wetu unakwenda taratibu sana, Mungu akanipa maono haya ya kuandaa nyimbo nyingi za Kiingereza na lugha zingine ili niweze kiwafikia," amesema





## IRENE ATOBOA SIRI YA UREMBO WAKE

MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Irene Paul, amesema mwonekano wake unazidi kuvutia kutokana na kujilinda na matumizi ya vipodozi vyenye kemikali.

Amesema kwamba kujipenda mwenyewe kwa kutumia vitu asilia vya kung'arisha ngozi ni jambo analozingatia kila kukicha.

"Nikitaka kuoga ni lazima natumia maji safi, sabuni na mafuta yanayotokana na vitu vya asili. Ni lazima kujipenda mwenyewe kabla ya watu kukusifia," amesema Irene





## Mwijaku unataka Diamond akukere

MTANGAZAJI na chawa maarufu, Mwijaku amemkabili mwanamuziki Diamond Platnumz, akimshauri kuacha kuachia ngoma yake mpya siku ya Ijumaa ambayo ni maalum kwa ibada kwa waumini wa Kiislam.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Mwijaku amesema Diamond Platnumz, amekosea kutangaza kuwa ataachia wimbo mpya 'Zuwena' siku ambayo wengi wapo kwenye ibada.

"Kesho Ni siku ya Ibada Ijumaa,wewe ni Muislam unaachiaje Nyimbo? Tukutane Msikitini Mwambino," ameandika Mwijaku.

## HATA ZAMANI 'SIMBA, TEMBO' WALIKUWEPO

**Na Adam Fungamwango**

WANAMUZIKI na wasanii ni watu ambao wanazifanya jamii kuburudika na wakati mwingine kusahau shida zao kwa muda.

Kutokana na wanamuziki kufanya kazi ya kuwatuliza watu na kuwaburudisha, wamejikuta wakipewa majina ya utani na mashabiki ambayo yamekuwa yakiwakaa vema wakati mwingine na kuwa kama majina yao asilia.

Inafikia wakati hata majina yao halisi husahaulika na badala yake majina yao ya utani waliopewa na mashabiki ndiyo yanayovuma.

Mfano Abdul Nasseb, maarufu kama Diamond Platnumz, amepewa jina la mnyama Simba, na mpinzani wake kimuziki Harmonize, yeye akapewa jina la 'tembo' na mashabiki. Hii siyo leo tu, bali hata zamani ilikuwepo.

Leo tunaangalia wanamuziki waimbaji ambao kutokana na kazi yao nzuri, wakapachikwa majina ya ndege, pamoja na wanyama.

**Hemed Manerti 'Chiriku'**

Huyu ni kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz Band, iliyokuwa maarufu mno miaka katikati ya miaka ya '70, hadi mwanzoni mwa '90.

Alikuwa mwimbaji tegemeo na mtunzi wa bendi hiyo kiasi cha kuifanya kuwa maarufu na yenye mashabiki wengi. Kutokana na umahiri wake, mashabiki wake na wa muziki wa dansi kwa ujumla wakampachika jina la 'Chiriku' wakimfananisha na ndege huyo kutokana na sauti yake na uimbaji wake.

**Jerry Nashon 'Dudumizi'**

Ni mtunzi, mwimbaji mahiri wa bendi za Vijana jazz na Bima Lee, bendi ambazo alizitumikia kwa muda mrefu hadi kifo chake mwaka 1995.

Alikuwa mahiri mno kwa nyimbo za mapenzi, akizipamba kwa maneno ya mahaba na ya kubembeleza, kiasi cha kuwa maarufu nchini na mashabiki kumpachika jina la 'Dudumizi." Hii ni kutokana na sauti yake nzito ya kitetemeshi, iliyofanana sana na ndege huyo ambaye akilia ni kama maji yanamiminwa kwenye glasi.

**Mohamed Salum 'Gotagota'**

Alikuwa ni mwimbaji wa sauti ya kwanza kali kwenye bendi za Tabora Jazz, Mwenge Jazz na Vijana Jazz. Si wengi wanamfahamu kwa jina lake halisi, ila ukisema Gotagota kila mmoja atajua unamzungumzia nani pamoja na kwamba naye ni marehemu. Alipewa jina hilo alifananishwa na ndege gotagota mwenye mdomo mrefu anayegongagonga miti na kutoa sauti fulani ambayo ndiyo inayofananishwa na uimbaji wa mwanamuziki huyo.

**Nana Njige 'Nana Mzuri'**

Mwimbaji wa kike wa bendi za Super Rainbow, Washirika Tanzania Stars na Magereza. Jina lake ni Nana Njige. Lakini mashabiki wake kwenye muziki wakampachika jina la 'Nana Mzuri'. Nana ni ndege mmoja mwenye wajihi mzuri kwa rangi ya manyoya yake na muonekano. Na alipewa jina hilo kutokana na urembo wake. Mwanamuziki huyo ambaye ameshafariki dunia alitamba sana kwa kibao cha 'Ashura' akiwa na Magereza Jazz.

**Wilson Peter 'Kinyonga'**

Kiuhalisia ni kwamba Kinyonga si jina lalisi la wanamuziki wa Kitanzania , Wilson Peter na mdogo wake Gorge Peter, waliokuwa na bendi ya Jamhuri Jazz ya Tanga, kabla ya kuunda bendi yao ya Arusha Jazz na kuvuka mpaka kuingia nchini Kenya na kuibadilisha na kuiita Simba Wanyika.

Wilson ndiye aliyepewa jina la Kinyonga na mashabiki wake, lakini kutokana na jina hilo kuwa maarufu zaidi, baadhi walidhani ni jina la ukoo kiasi hata mdogo wake George naye kuitwa hivyo.

Kwa hiyo wote wakawa jina la mwisho wanaishia na Kinyonga. Kinyonga ni mnyama mdogo anayefanana na mjusi na anayetembea taratibu na kujibadilisha rangi.

FILAMU

## Tatizo simu: Fundi simu mbabaifu

**Na Adam Fungamwango**

UKIWA unafanya kazi yoyote kuwa makini, vinginevyo unaweza kusababisha matatizo makubwa. Kuna kazi zingine kama udaktari, dereva, unahidha au urubani ukifanya kosa dogo tu linaweza kusababisha kuua abiria.

Injinia anaweza kusababisha ghorofa kuanguka. Zipo hata kazi ndogo tu ambazo zinaonekana kuwa za kawaida sana na hata kama anayezifanya akikosea hazitoleta madhara, hii si kweli.

Ukitaka kujua hilo hebu ifuate filamu hii ni makini, kuna kitu unagundua na kujifunza. Filamu inaitwa 'Tatizo Simu', imechezwa na Mary Juma, Kiango Mohamed, Sabrina Kilimila na wengineo. Pumba ni mwanaume anayeshi vema na mkewe Sabra.

Siku moja simu ya mkwe ikawa mbovu, akaichukua na kuipeleka kwa fundi Kobe. Pamoja na kulipia, lakini hakuwa na muda wa kuipeleka nyumbani hakuwa nao. Pumba anafanya biashara ya kuuza genge, hivyo akamtuma rafiki yake Zongo kuipeleka kwa mkewe.

Zongo anafanya kama alivyoagizwa. Anafika kwa shemeji yake na kumkabidhi simu. Alipoondoka tu, simu zikaanza kupigwa.

Sabra anaweka sikioni akasikia sauti na mwanamke mmoja aliyejaaliwa kuongea kama cherehani. Mwanamke huyo hamezi mate, akaongea mfululizo.

"Ndiyo nilikuwa nakutaka wewe, mwanamke usiokuwa na haya, mwanamke usiejua kumlea bwana, mwanamke usiyejua kumlea mume, unajifanya bwana wa kwako peke yako, unajiifanya na wewe umepaaata, sasa ninavyokueleza bwana ninaye mimi, bwana najua anaoga nini, najua anakula nini, najua avae vipi. Mwanamke usiyependeza sketi wala suruali, mwanamke, hupendezi sokoni wala super market, usiyejua wanja wala 'lip stick', usiyejua bwana anataka mahaba ya namna gani. Huna haya, usiyejijua, usiyejitambua. Unisikie vizuri na masikio yako yasikie, mwanamke usiyejua kulea mwanaume, usiyejua kumnyenyekea bwana, mwanamke usiyejua mahaba..." Hakuendelea tena kuvumilia kuchambwa. Alikuwa anatetemeka kwa maumivu, wivu, uliochanganyikana na hasira. Akaiweka simu chini asikikie kitu.

Tayari akawa amejua kuwa mumewe ana mwanamke mwingine huko nje. Kwanza anamfuata Zongo na kumpa vipande vyake kuwa yeye na mumewe lao moja. Halafu akarudi nyumbani, akafungasha kilicho chake na kwenda kwao.

Zongo akamfuata Pumba na kumwambia shemeji amegundua kuwa ana nyumba ndogo. Ni kweli Pumba ana nyumba ndogo. Kwa hasira akaenda huko na kumuwakia hawara yake kwa nini amempigia simu mkewe na kumtukana. Hawara, anaapa na miungu yake yote kuwa hajafanya kitu hicho. Penzi hapo hapo likaisha. Lakini Pumba akawa amekosa mke. Ameshakwenda kwao.

Baada ya wiki kadhaa za misukosuko, kikawekwa kikao cha usuluhusi ambacho bado kilikuwa kigumu. Wakati wakiwa kwenye kikao, fundi Kobe alikuwa na mteja mmoja wa kike. Akadai kuwa alibadilisha simu. Akadai ile simu aliyompa Zongo na ikapelekwa kwa Sabra ni ya mteja aliyekuja naye, aliibadilisha kimakosa. Mkononi alikuwa na simu yenyewe na mke wa Pumba.

Kila mtu akapatwa na mshangao. Ina maana alichokuwa akisikia Sabra na yale yote hayakuwa ya kwake.

Alikuwa akipiga mwanamke mwingine kumpigia mwingine na siyo yeye. Mumewe hahusiki na hilo. Ndoa ikaponyeshwa.



## Amber Rose kama kweli vile

MWANAMITINDO Amber Rose amefunguka kuwa hataki kuolewa tena katika maisha yake yote.

Rose alifichua kuwa tangu awe na wanaume wengi, hakuna kilichobadilika.

Awali alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Kanye West, 21 Savage, na mume wa zamani Wiz Khalifa.

Anadai kuwa wanaume wamekuwa na tabia ya kuchukiza baada ya muda, na hivyo hataki tena uhusiano wowote nao.



## Pere kumbe ulianza zamani

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Naija, Pere Egbi, ameibua mjadala kwa mashabiki zake baada ya kudai alioa akiwa na umri mdogo.

Pere amefichua katika mahojiano yake na Toke Makinwa, akiweka wazi kwamba alioa akiwa na umri wa miaka 25.

"Nilioa nikiwa na umri wa miaka 25, kwa mwaka mmoja na ilikuwa ni mapenzi ndani ya gari kutokana na kutokuwa na makazi nilipohamia Marekani," amesema.


## Buju aibua mjadala

MWIMBAJI nyota kutoka Nigeria. Buju BNXN ameibua mjadala baada ya kuvuja maongezi yake na Davido, akionekana akimshukuru kwa kumsaidia.

Katika mazungumzo hayo, Buju alionekana akimpongeza Davido kwa kuwasili salama safari yake.

Buju alibainisha kwamba Davido alimkumbuka sana kutokana na usaidizi wake katika kipindi muhimu.





## Temi afurahia miaka 6 kwenye ndoa

MWIGIZAJI wa Nigeria, Temi Otedola, ametimiza miaka sita ya kukutana na mchumba wake, Eazi.

Binti huyo wa mfanyabiashara bilionea aliandika kwenye Instagram kwamba anasherehekea kumbukumbu ya kuwa katika ndoa kwa miaka sita.

"Jana tulikuwa na furaha baada ya kukutana miaka sita iliyopita," aliandika kwenye ukurasa wake wa Istagram.

## 2Baba amkumbuka EMD kiaina

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Innocent Idibia, anayejulikana kama 2baba, amemwagia sifa msanii wa filamu wa Nollywood, Richard Mofe Damijo, maarufu kama RMD.

Mwimbaji huyo mkongwe alionyesha mapenzi yake kwa muigizaji huyo katika chapisho lake la Instagram alimwelezea kuwa kama mtu anayemheshimu.

2baba aliandika kwamba hakuna mtu anayemkubali zaidi kama mwigizaji huyo mashuhuri wa Nollywood.







# Mradi ujenzi bomba mafuta waanza rasmi

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

UJENZI wa awali wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), umeanza rasmi katika eneo la Chongoleani, mkoani Tanga, baada ya Kampuni inayotekeleza mradi huo, kuandaa eneo la ujenzi wa matangi, jeti, miundombinu ya bandari na makazi ya muda ya wafanyakazi.

Inakadiriwa mapipa 216,000 ya mafuta ghafi yatasafirishwa kwenye bomba hilo kwa siku moja kutoka Uganda kwenda kwenye Peninsula ya Chongoleani nchini Tanzania, ambako yatajengwa matangi ya kuhifadhia mafuta, kabla ya kupakiwa kwenye meli na kwenda kuuzwa katika soko la dunia.

Mkurugenzi wa Petroli wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Gerald Maganga, alisema jana kuwa serikali ya Tanzania, inaridhishwa na hatua za awali za uandaaji wa utekelezaji wa mradi huo mkubwa.

Maganga alisema hayo alipokuwa akizungumza na ujumbe wa maofisa wa Mamlaka ya Petroli ya Uganda (PAU), walioongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wake, Ernest Rubondo, baada ya kutembelea na kukagua hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo.

"Tumeona maeneo mbalimbali yakiandaliwa, kwa ajili ya kujenga matanki na miundombinu mingine. Tumefurahishwa hasa na namna wanavyozingatia ushirikishwaji wa wazawa katika kufanya kazi mbalimbali.

"Kazi inaridhisha na inakwenda vizuri. Matumaini yetu ni kwamba muda uliopangwa kukamilisha ujenzi huo, utakwenda sawa kama ilivyotarajiwa," alisema Maganga

Kutokana na umuhimu wa mradi huo, mkurugenzi huyo amewashauri Watanzania, wakiwamo watoa huduma za ukandarasi, kujiandikisha kwenye kanzidata ya EWURA ili kupata fursa ya kunufaika na kazi mbalimbali za utoaji wa huduma, wakati wa ujenzi wa mradi huo. Baada ya ukaguzi huo, Rubondo alipongeza hatua iliyofikiwa, huku akieleza matumaini yake katika maendeleo ya ujenzi wa bomba hilo la mafuta ghafi la Afrika Mashariki.



Ofisa Afya wa mkoa wa Tanga, John Sagaika (kushoto), akizungumza wakati wa kikao kazi cha kuijengea uwezo kamati ya hamasa na mawasiliano dhidi ya magonjwa ya mlipuko ya mkoa huo, iliyofanyika mjini Muheza jana. Waliokaa mstari wa mbele (kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Juma Irando. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wadau wa utalii wawakumbuka wahitaji

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WADAU wa shughuli za utalii kutoka Kampuni ya Masai Wounders ya jijini Arusha, wamewakumbuka wanafunzi 1,544 wa Shule ya Msingi Matimu na Sekondari ya Mukulat zilizoko Halmashauri ya Arusha, waliokuwa na uhitaji wa sare za shule na vifaa vingine vya kiada.

Wanafunzi hao wamenufaika pia na jozi 1,300 za viatu, mashati, sketi, suruali, masweta, nguo za michezo, vifaa vya michezo na vitabu vya kiada.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Ang'weni Lang'o, alisema wameguswa kugawa vifaa hivyo, baada ya kuona tatizo linalowakabili baadhi ya wazazi kushindwa kumudu kuwapatia watoto wao mahitaji ya shule.

Alisema kutokana na tatizo hilo, kampuni hiyo ilifikia uamuzi wa kubeba jukumu hilo la kuwapunguzia mzigo wazazi ili wanafunzi hao wapate nafasi ya kuhudhuria masomo bila kuwapo kwa kikwazo chochote.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Elizabeth Ngobei, aliishukuru kampuni hiyo, kwa kutoa msaada huo, ambao utakwenda kuwa chachu ya maendeleo katika sekta ya elimu. Aidha, aliwasihi wanafunzi wa shule hiyo kusoma kwa bidii, kwa kuwa tayari wadau hao wa elimu wametimiza wajibu na majukumu yao.

Kadhalika aliwataka wanafunzi kutambua kuwa wako watoto wenzao wanaoshindwa kuhudhuria shule kwa kukosa vifaa vya shule hivyo, aliwasisitiza kuthamini msaada waliopatiwa kwa kuongeza bidii katika masomo ili kufikia ndoto zao.

"Wazazi mna jukumu la kuwasimamia watoto hawa kutunza vifaa hivi, lakini pia walimu mna wajibu wa kuhakikisha mnawafundisha wanafunzi ili waweze kufaulu vyema na kufikia malengo yao," alisema Ngobei. Upendo Paulo, mwanafunzi wa darasa la sita, alisema ndoto yake ni kuwa daktari, hivyo aliahidi kusoma kwa bidii kutimiza ndoto yake kama ilivyo kwa wanafunzi wengine wanaosoma shule binafsi zenye mchepuo wa kiingereza.

Baada ya makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Matimu, Philemon Loth, aliwashukuru wadau hao, kwa mambo makubwa wanayoyafanya kwenye shule hiyo, akiahidi kushirikiana na walimu kuhakikisha watoto wanahudhuria shuleni na kufanya vizuri katika masomo.

# Mamuya atoa neno wazee ombaomba

**Na Asraji Mvungi,** ARUSHA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi (NEC), Halima Mamuya, amesema idadi kubwa ya wazee wanaofanya kazi ya 'ombaomba' hivi sasa barabarani katika viunga mbalimbali vya jiji la Arusha, walikuwa na maisha mazuri.

Akizungumza na wazee katika kikao kazi cha kutathmini matatizo yao, Mamuya alisema licha ya ombaomba kuongezeka kila uchao katika jiji la Arusha, bado serikali ina uwezo wa kulipatia ufumbuzi na kwamba kinachotakiwa ni utayari wa kuyashughulikia pamoja na ushirikiano kutoka kwa wazee wenyewe.

"Asilimia kubwa ya wazee wanaoonekana ombaomba kwa sasa, walikuwa na maisha yao mazuri tu. Kuna mambo mengi yaliyochangia kuwafikisha hapo, mengine yako nje ya uwezo wao na mengine yanachangiwa na mazingira na mfumo wa maisha waliokuwa wanaishi, kabla ya kufikia umri huo na kujiingiza kuombaomba.

"Kuna wengine wana matatizo yanayotokana na kukosa ushauri mzuri na maandalizi mazuri wakiwa bado vijana. Lakini pia kuna wengine wana matatizo yanachangiwa na familia zao kutowajali wazee," alisema.

Katika kikao hicho, Katibu wa Umoja wa Wazee wa Jiji la Arusha, Salim Mvungi, alisema licha ya kuwepo kwa mikakati mingi ya kuwasaidia wazee, utekelezaji wake kwa vitendo bado ni mdogo na hauridhishi.

"Ongezeko hili la wazee ombaomba, iko haja ya serikali ikaangalia upya namna ya kulisaidia kundi hili kujinasua katika aibu hii. Kundi la wazee, kama yalivyo mengine linahitaji kutazamwa kwa jicho tofauti, na kama ambavyo makundi mengine yamekuwa yakipewa upendeleo na uwezeshaji. Hata wazee nao wanauhitaji," alisisitiza Mvungi

Alipotafutwa kutoa picha juu ya ufumbuzi wa tatizi hilo, Meya wa Jiji la Arusha, Dk. Maxmillian Irange, alisema ongezeko la tatizo hilo linachangiwa na sababu mbalimbali,ikiwamo mmomonyoko wa maadili, utandawazi na mifumo ya maisha.

Kwa mujibu wa Meya huyo, Halmashauri ya Jiji hilo, inaendelea kutekeleza sera na miongozo ya serikali, juu ya huduma kwa wazee, ikiwemo kupata matibabu bure.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Zama za mwiko mtoto mdogo kula firigisi, mjamzito mayai

**Na Adam Fungamwango**



KILA nchi duniani, ina sheria zake, taratibu na utamaduni wake ambao unaweza kufanana au kutofautiana na zingine.

Kwa hiyo mbali na sheria, lakini watu wa nchi husika wanaweza kuwa na utaratibu wao wa kimaisha na utamaduni ambao ama ni wa asili au uliwekwa na mababu tangu enzi na enzi, ukirithishwa vizazi kwa vizazi.

Mfano mdogo tu ni kwamba Watanzania wanafuata sheria zilizowekwa na nchi ambazo zimetungwa na kupitishwa bungeni, bila kujali majiji, mikoa, wilaya au vijiji.

Lakini kuna utaratibu na utamaduni wa watu wa mkoa wa Kagera ambao unatofautiana na watu wa mkoa wa Rukwa. Hata chakula, wengine chakula chao kikuu ni ndizi na wengine ugali.

Tukienda mbali zaidi hata makabila yana utamaduni wao, kuanzia mtoto anapozaliwa nini anatakiwa kufanyiwa, anapopevuka, kuoa na hata mtu anapofariki. Kila kabila na taratibu zake.

Hata baba huweka utaratibu wa kuiendesha familia yake ambao haufanani na nyumba nyingine. Baba huyu anaweza kuweka utaratibu wa saa mbili tu usiku watoto wake wawe tayari ndani wamelala, mwingine mpaka saa sita usiku, bado watoto wanaagalia TV.

Miaka ya nyuma babu na baba zetu walikuwa na utaratibu wao ambao ulienea nchini nzima wa kutengeneza kama sheria isiyokuwa rasmi, utamaduni na utaratibu wa maisha ambao uliwafanya watoto wengi wakati huo kuishi kwenye msitari ulionyooka.

Sijawahi kusikia popote kama walikaa kikao au kutengeneza mifumo hiyo, lakini nadhani nao walirithi kutoka kwa mababu na baba zao nao kurithisha watoto wao.

Kwa sasa utaratibu huo ni kama unakufa kifo cha asili kutokana na maendeleo ya teknolojia ambayo yanawafanya watoto wengi kuwa werevu zaidi.



Pamoja na kwamba kuna wakati wazee wa zamani walionekana kama wakali kupita kiasi, au waliweka mifumo na mikwara ya uonevu, lakini ilisaidia mno kwenye malezi, watoto kupendana, kuwa na heshima na binadamu wote, na hofu ya Mungu.

Waliweka taratibu nyingi ambazo kwa sasa zinaonekana kama vichekesho na zilizopitwa wakati. Ni kweli baadhi zimepitwa na wakati, lakini nyingine zilihitajika kuendelea hadi leo.

Kama nilivyosema wazee waliweka kama sheria ambazo hazikuwa na adhabu, bali mikwara na vitisho kwa yeyote ambaye atakiuka, wenyewe wakiita miiko.

Mfano, walimkataza mama mjamzito asile mayai mpaka pale atakapojifungua. Siyo kama walikuwa wachoyo.

Zamani haya mambo ya upasuaji yalikuwa bado sana na mtoto alikuwa anazaliwa nyumbani kwa msaada wa wakunga, hakukuwa na njia ya mkato ya upasuaji na hata hospitali zilipokuja, bado njia hiyo ilionekana ni hatari na ilikuwa ya mwisho kabisa baada ya kila kitu kushindikana.

Kwa maana hiyo, mtoto hakutakiwa awe ni mkubwa akiwa tumboni ili asimsumbue mama wakati wa kujifungua. Baadhi ya vyakula, ikiwemo mayai na nyama ya kuku, ilionekana kuongeza ukubwa na mtoto tumboni kwa kiasi kikubwa.

Hekima ya wazee wa zamani walikuwa wakiweka vitisho ambavyo vilimuweka mtu sawa kisaikolojia afuate misingi hiyo hata kama hakuna atakayemwambia hivyo tena.

Walisema mama mjamzito akila mayai, atazaa mtoto akiwa hana nywele, ambazo hazitoota tena na atakuwa kipara maisha yake yote. Sidhani kama kuna mama yeyote ambaye anataka mtoto wake awe kipara. Hapo hata iweje, hata mama huyo akienda Ulaya, hatokula mayai hadi ajifungue.

Baadhi ya miiko ni mtoto kula firigisi, nyama hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya baba tu. Mwiko mwingine ni watoto kunawa kabla ya wakubwa, mtoto kuwaruka wenzake, hakuruhusiwa mtoto kusimama pembeni au karibu na wakubwa au wenzako kwa sababu eti atawanyonya damu na miiko mingine mingi sana hatuwezi kuimaliza hapa.

Kama nilivyosema watu wa zamani walikuwa na hekima sana, kuzuia watoto kula mapaja na firigisi iliweza kudhibiti ulafi kwa watoto na si uchoyo. Mtoto anatakiwa ale kwa kiasi.

Kukataza kumruka mwenzio walilenga kuepuka ajali maana unaweza kuruka ukashindwa ukamuangukia ukaumia au ukamuumiza, kumwambia mtu eti mkono ukiwasha atapata hela walikuwa wanamtibu kisaikolojia, badala ya kuwaza sana juu ya tatizo awaze kitu kingine cha faraja, ukijikwaa kuna mtu amekusema vibaya kulilenga kuepuka kuwasema wengine vibaya kwani wangesababisha hatari kwa mwingine, na vijijini kulikuwa ni mwiko kwa baadhi ya miti kufanywa kuni labda kama msimu huo mvua haitanyesha, vinginevyo kwenye familia yenu kuna mtu mmoja atafariki dunia. Hii ililenga kutunza miti. Ukiwaambia watu tu marufuku bila mkwara kama huo, kuna mtu anaweza kufanya, lakini akifikiria kuna ndugu yake atakufa, thubutu, hawezi. Je unakumbuka miiko mingine unayoifahamu iliyowekwa na wazee wa zamani enzi hizo?

**Tuma meseji 0716 350534.**



# Kenyatta apunguziwa walinzi wa kumlinda

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa zamani wa Kenya, Uhuru Kenyatta, amepunguziwa ulinzi kwa kiasi kikubwa, huku uhusiano wake na Rais Willium Ruto ukizidi kuwa mbaya.

Wakati kiongozi huyo akipunguziwa idadi ya walinzi, kumeibuka miito ya kufanyika kwa uchunguzi dhidi ya utajiri mkubwa wa familia ya Kenyatta.

Mkuu wa polisi wa Kenya, aliwaambia waandishi wa habari kwamba mabadiliko hayo yamefuata mwongozo wa kanuni kuhusu usalama wa rais mstaafu.

"Yuko salama, chochote kilichofanyika kimefanyika kwa nia nzuri ," alisema Inspekta Mkuu wa polisi, Japheth Koome.

Usalama wa Kenyatta wenye walinzi 96 umepunguzwa hadi 25, huku mke wake akibaki na walinzi watano, limeripoti gazeti la Daily Nation.

Mawaziri wa zamani waliokuwa na ushawishi wakati wa utawala wa Rais Kenyatta, pia wamepunguziwa ulinzi wa kulinda usalama wao.

Washirika wa Rais Ruto, wametoa wito wa kufanyika kwa uchunguzi kuhusiana na kuondolewa ushuru wa familia ya rais wa zamani Uhuru Kenyatta wakati wa utawala wake.

Rais Ruto wiki hii alisema kuwa wakwepaji wa kodi ndio wanaodhamini mikutano ya hadhara ya hivi karibuni ya upinzani.

Wakati huo huo, mahakama nchini humo inatarajiwa kutoa hukumu kwa polisi watatu na raia mmoja wakishtakiwa kwa mauaji ya wakili maarufu wa masuala ya haki za binadamu Willie Kimani.

Polisi hao Fredrick Leliman, Stephen Cheburet, Sylvia Wanjiku na raia Peter Ngugi, walipatikana na hatia ya mauaji ya kimani, mteja wake Josephat Mwendwa na dereva wa teksi Joseph Muiruri.

Miili ya Kimani na watu wengine wawili ilipatikana baaya ya kutupwa mtoni katika viunga vya mji mkuu wa Nairobi.

Kimani , Mwendwa na Muiruri walionekana kwa mara ya mwisho tarehe 23 Juni 26 kwenye kituo cha polisi.

Miili yao iliyokatwakatwa iligundulika wiki mbili baadaye katika mto ulioko kilomita 100 kutoka mji mkuu.

Hukumu hiyo inakuja wakati huduma ya polisi nchini Kenya ikichunguzwa zaidi kuhusiana na mauaji ya kiholela na utekaji nyara. Rais William Ruto tayari amevunja vikosi kadhaa maalum vya polisi vinavyoshutumiwa kwa mauaji na utekeji wa raia.

**BBC**



Papa Francis, akitazama onyesho alipohudhuria mkutano wa vijana na makatekista kwenye uwanja wa Stade des Martyrs wakati wa ziara yake Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. **PICHA: REUTERS**

# Marekani yahofia puto linaloshukiwa kuwa la China

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imesema inafuatilia puto linaloshukiwa kuwa la China ambalo limeonekana likiruka kwenye maeneo nyeti katika siku za hivi karibuni.

Maofisa wa ulinzi walisema wana uhakika puto hilo la uchunguzi wa hali ya juu ni kutoka China, ambalo lilionekana likiruka juu ya anga la jimbo la magharibi la Montana, nchini humo.

Hata hivyo, viongozi wa kijeshi waliamua kutoliangusha kwa kuhofia kuanguka na kusababisha madhara.

Hata hivyo, China bado haijatoa jibu kwa tuhuma hizo.

Rais wa Marekani Joe Biden amefahamishwa kuhusu kifaa hicho.

Kitu hicho kiliruka juu ya Visiwa vya Aleutian vya Alaska na kupitia Canada kabla ya kuonekana juu ya jiji la Billings huko Montana siku ya Jumatano.

Ofisa mkuu wa ulinzi akizungumza kwa sharti la kutotajwa jina, alisema serikali ilitayarisha ndege za kivita, zikiwemo F-22, endapo Ikulu ya White House itaamuru kitu hicho kiangushwe.

Viongozi wakuu wa kijeshi, akiwemo Waziri wa Ulinzi, Lloyd Austin na Jenerali Mark Milley, mwenyekiti wa Wakuu wa Pamoja wa jeshi la Marekani, walikutana Jumatano kutathmini tishio hilo.

Montana, jimbo la magharibi lenye wakazi wachache, ni nyumbani kwa mojawapo ya maeneo matatu pekee ya kuhifadhi makombora ya nyuklia nchini humo, katika Kambi ya Jeshi la Wanahewa ya Malmstrom, na maofisa walisema chombo hicho cha kijasusi kilikuwa kikiruka juu ya maeneo nyeti kukusanya taarifa.

Ofisa wa ulinzi, hata hivyo, alisema hakuna tishio la ujasusi lililofanikiwa kwa sababu maofisa wa nchi hiyo wanajua puto hilo liko wapi na linapita wapi.

Aliongeza kuwa pia hakuna tishio kwa usafiri wa anga wa kiraia kwani kifaa hicho kilikuwa kwa kiasi kikubwa kipo juu ya urefu unaotumiwa na mashirika ya ndege ya kibiashara.

**BBC**

## Wanamgambo wawili wauawa Pakistan

**KARACHI,** PAKISTAN

JESHI la Pakistan limevamia maficho na kuua wanamgambo wawili wa kundi laTaliban la Pakistan.

Msako huo umefanyika karibu na mpaka na Afghanistan jana, na kusababisha kutokea majibizano ya risasi.

Waziri mkuu wa Pakistan, Shahbaz Sharif, aliimuita kiongozi wa upinzani nchini humo kujibu kuhusu kuongezeka kwa matukio ya vurugu, ikiwa ni pamoja na tukio la mlipuko wa bomu lililotokea msikitini na kuua watu 101.

Jeshi liliongeza kuwa wamegundua shehena ya silaha katika maficho ya wanamgambo hao Kaskazini mwa Waziristan, katika mkoa wa Pakhtunkhwa.

Taliban wa Pakistan ni kundi tofauti lakini ni washirika wa Taliban wa Afghanistan, walionyakua mamlaka nchini Afghanistan mwaka mmoja uliopita.

**DW**

## Wahamiaji 46 waokolewa

**ROMA,** ITALIA

WALINZI wa pwani ya Italia wamewaokoa wahamiaji 46 pamoja na miili ya watu 8 ikiwemo mwanamke mmoja mjamzito

Tukio hilo lilitokana na boti waliyokuwa wakisafiri watu hao kuonekana kwenye eneo la bahari ya kisiwa cha Malta.

Kulingana na shirika la habari la ANSA chombo hicho kilionekana wakati kikikaribia kufika kwenye kisiwa cha Lampedusa kusini mwa Italia.

Ndani yake kulikuwa na wahamiaji hao kutoka mataifa ya Kaskazini mwa Afrika na wengine walipoteza maisha.

Kila mwaka maelfu ya wahamiaji kutoka Afrika Magharibi na Kaskazini hufanya safari hatari kujaribu kuvuka bahari ya Mediterannia ili kutafuta maisha bora kwenye mataifa ya Ulaya.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ARRANT BUSINESS SOLUTIONS COMPANY LTD

**Notisi/Tangazo la mnada wa hadhara**

Kwa idhnin tuliyopewa na jitihada **saccos ltd (REG KAR 689)** tunatoa notisi ya kulipa madeni yenye dhamana tajwa hapo chini ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili, vinginevyo tunafanya mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| Jina la mdaiwa | Mali iliyowekwa dhamana | Mahali ilipo | muda |
|---|---|---|---|
| Richard Philipho | Nyumba/shamba na mabanda ya biashara | Nyakahura | Kuanzia saa 4 kamili asubuhi |

**Masharti ya mnada**

Dhamana zitauzwa kama zilivyo

- Mnunuzi anatakiwa kulipa asilimia 25% siku ya mnada na asilimia 75% siku kumi na nne toka siku ya mnada.
- Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% kwa muda uliopangwa hatorudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa.
- Gharama zote za kubadilisha hati miliki na gharama nyingine zitakuwa juu ya mnunuzi

**Mawasiliano zaidi piga simu 0654132285**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALES PAUL BWANAKUNU**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye usajili **MC 203 CKH.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**WMB/RB/321/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMMED ALI RASHID**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: **T358 DYZ.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**DAR/KIL/RB/47738/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MORLAND M MATTOWO**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 528 ACA** aina ya **TOYOTA- PRADO,** Chasis No. **KZJ950048159,** Engine No. **IKZ0454248.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **MWA/NY/RB/44631/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALBERT PETER MASAO**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 509 DEY** aina ya **TOYOTA- HAICE,** Chasis No. **RZH1241001696,** Engine No. **IRZ3154470.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **MWA/NYA/RB/46577/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – LA MWANZA**

**MAOMBI Na.20 YA MWAKA 2021**

**COSTANTINE MNAKA...............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **MARTHA JOSEPH MTUI (Sued as Guardian of PROSPERVICTOR FABIAN MASAGA (Minor)**
2. **DAVID G. MAGANGA**
3. **THOMAS CHARLES KILATU**

**......WAJIBU MAOMBI**

**WITO WA BARAZA**

**KWA,**
**THOMAS CHARLES KILATU,**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba MKoa wa Mwanza, Ombi hili limepangwa kusikilizwa tarehe 06/02/2023 katika chumba namba 3 cha Baraza , Barabara ya Airport jengo liko mkabala na Mahakam ya Mwanzo Mwanza Mjini, Tanzania.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi/ shauri hilo linalokukabili.

KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika kwakosiku hiyo, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo

Imetolewa name kwa Amri na Lakiri / Mhuri wa Baraza leo tarehe 2/2/2023

MURIRYA N.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MWANZA.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**

**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Madai Na.01/2023**

**Jins la Mdai BIOSUSTAIN(T)LTD**

**Jina la Mdaiwa .FALE GEORGE NA WENZAKE WAWILI(2)**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa NKUBA MIZUMARI,**
**WA KIJIJI CHA BUGARAMA,MASWA.**

**K.K AFISA MTENDAJII,**
**KIJIJI CHA BUGARAMA**
**MASWA.**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba(Eleza hapa habari za Madai). Anawadai wewe pamoja na wenzako wawili pesa Sh 22,710,700/-zikiwa ni pesa za ununuzi wa Pamba msimu wa 2022/2023. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 08 Mwezi 02 Mwaka 2023 saa 2;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 31Mwezi 01 Mwaka 2023.

HAKIMU

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

---

**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Madai Na.01/2023**

**Jins la Mdai BIOSUSTAIN(T)LTD**

**Jina la Mdaiwa .FALE GEORGE NA WENZAKE WAWILI(2)**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa FALE GEORGE**
**WA KIJIJI CHA MWABARATULU,MASWA.**

**K.K AFISA MTENDAJII,**
**KIJIJI CHA MWABARATULU,**
**MASWA.**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba(Eleza hapa habari za Madai). Anawadai wewe pamoja na wenzako wawili pesa Sh 22,710,700/-zikiwa ni pesa za ununuzi wa Pamba msimu wa 2022/2023. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 08 Mwezi 02 Mwaka 2023 saa 2;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.

Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 31Mwezi 01 Mwaka 2023.

HAKIMU

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

---

**3FORM58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.18 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BUPE SAMSON MWAKASEGE**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**
**BARAKA ASANGALWISYE MASIKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of 02, 2023

Dated at DAR ES SALAAM this **17 day of 01, 2023**

..........................................
Senior Resident Magistrate

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 1173 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GENOVEVA KOKUHIKIJANYIA ISHENGOMA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTER OF ADMINISTRATION BY**
**HELLEN DONATUS ISHENGOMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 21 Day of 02, 2023

**Dated at DAR ES SALAAM this 02 day of 02, 2023**

..........................................
Senior Resident Magistrate




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# MTAKE MSITAKE-17

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na umbali huo, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja wa wasichana warembo katika kijiji hicho anayepata shida hiyo. Hawana mahali kwa kupeleka malalamiko, wala wa kumlalamikia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

**MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa kiburi baadhi ya viongozi wa kijiji kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yanayopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, msichana mrembo kijijini hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.**

****************************************




Ofisa yule aliyekuwa kwa DJ na MC, bado aliendelea kuongea maneno ambayo kwa asilimia zote yaliwafurahisha wanakijiji cha Maweni.

"Wakati tunaendelea na hili, sisi kama maofisa wa serikali, tumesikitishwa sana na kitendo kilichotokea huku cha mmoja kati ya wageni kwenye kijiji chenu kumwagiwa tindikali kiasi cha kupofuka macho. Nimesema kila kitu nilichokuwa kinafanyika huku kuna watu walikuwa wanatupa taarifa humu humu kijijini. Kwa maana hiyo yeyote aliyefanya hivyo ni lazima hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake. Na kama tulivyojua kila kitu kuhusu uwekezaji feki wa Usonzo, tunamjua aliyefanya hivyo, wala hatutaki kumuuliza mtu, tuna ushahidi wote. Tunajua kuwa kijana huyo yupo hapa na tunamuomba aje huku kwenye kipaza sauti ili tumuulize mswali kadhaa mbele yenu, kabla ya kumkamata mhusika."

Hapa kidogo wanakijiji walibaki kimya. Kila mmoja alikuwa anajua Mary ndiye aliyefanya hivyo. Na amekiri mbele ya hafla hiyo kabla ya maofisa hao kufika. Kila moja alikaa makini kuona nini kinatokea.

**"Adel, Adel, Adel.." Zilisikika sauti. Kuna baadhi ya vijana wachache ambao walikuwa wanataka kupanda jukwaani, lakini walizuiwa na walinzi.**

Adel alinyanyuka na kumuacha Mary pembeni yake aliyekuwa amejiinamia. Alianza kujikokota na kujipeleka mbele akitumia fimbo yake kupapasa. Alikuwa amevaa shati lake jeusi, suruali ya bluu na viatu vyeusi, akipiga miwani yake myeusi pia. Safari hii hakuongozwa na Mary kama ilivyokuwa kawaida ya wanakijiji walivyozoea. Akafika kwenye jukwaa la MC na DJ wake, akapewa kipaza sauti kingine kwa ajili ya maswali.

"Unaitwa nani?" Ofisa aliuliza.

"Naitwa Adel Adam."

"Una muda gani kwenye kijiji hiki?"

"Unakaribia mwaka sasa."

"Ulikuja kufanya nini kwenye kijiji hiki?"

"Nilikuja kumchukua bibi yangu mgonjwa, lakini kwa sababu nilimkuta akiwa yupo hoi sana haikuwezekana kumchukua, ikalazimu kumpeleka kwenye Zahanati ya jirani na kwa bahati nzuri akapata nafuu, lakini baadaye bibi mwenyewe aligoma kwenda mjini, mimi mwenyewe nikapata matatizo chungu nzima," akajibu Adel.

"Na huo upofu?"

"Umetokana na mambo yaliyojitokeza hapa."

"Nani amekutia huo upofu?"

"Dada mmoja amekaa pale anaitwa Mary."

"Jamani Mary yupo hapa?" Akauliza ofisa yule na kufuatiwa na vidole kutoka kwa watu waliokusanyika wakimuonyesha dada aliyekuwa ameketi kwenye kiti cha pembeni kwa Adel.

"Askari naomba ukae karibu ya huyo dada. Huyo tutaondoka naye mkutano ukiisha, msimfunge pingu, wala kumfanya chochote." Akasema Ofisa yule. Akanyamaza kidogo na kukawa na minong'ono ya hapa na pale.

"Jamani chakula si kipo na vinywaji vipo?"

"Ndiyooo"

"Endeleeni n vingine vitaletwa muda si mrefu kwa sababu mkutano huu ni mrefu na muhimu sana kwenye kijiji chenu cha Maweni. Jamani niseme nisiseme?" Akauliza Ofisa yule ambaye alionekana ni mcheshi na anayejua kuzungumza na hadhira.

"Semaaa" Akaitikiwa.

"Ni hivi, aliyesababisha yote haya hadi sisi kuja hapa. Aliyekuja hapa kijijini na kuyakuta madhila yenu yote na kutupatia tuje kusawazisha ni Adel."

Badala ya kushangilia, ukazuka ukimya wa ghafla ambapo ilionekana kabisa wanakijiji walishtushwa na taarifa hiyo ukiambatana na mshangao. Nusu dakika baadaye minong'ono ilianza.

"Adel ndiye shujaa wenu. Yeye ndiye alifanya kazi kubwa sana ya kutupatia kila kitu kinachofanyika, kuanzia mlivyokuwa mmenyang'anywa ardhi kitapeli, na taarifa zote za kunyanyaswa na hadi sisi kuja huku. Alikuwa kila siku asubuhi na jioni akitupatia nini kinaendelea na ndiyo maana niliwaambia kila kitu kilichofanyika huku na uhusika mkuu wa Mosha Usonzo na Mwenyekiti wenu Mzee Chale ambaye ameshatiwa nguvuni na wapo kwenye gari.

Kifupi niwaelezee kuwa Adel ni Ofisa Usalama Makao Makuu, Dar es Salaam aliyetumwa kuja kuifanya kazi hii na ameifanya kwa kiwango cha hali ya juu sana."

Vilisikika vigelegele kutoka kwa akinamama na mayowe wakimshangilia Adel, kijana ambaye wamekaa naye kiasi cha mwaka mmoja kasoro hivi.

"Adel, Adel, Adel.." Zilisikika sauti. Kuna baadhi ya vijana wachache ambao walikuwa wanataka kupanda jukwaani, lakini walizuiwa na walinzi.

Hata hivyo kuna wengine walishangaa kuona ofisa mzima kama huyo aliyefanya kazi kubwa, lakini akajiingiza kwenye mapenzi na msichana Mary kiasi cha kumwagiwa tindikali, akawa kipofu.

'Mwaka mmoja uliopita mama yake mzazi ambaye ni mwenyeji wa huku alifika na kujionea madudu haya ya uwekezaji mbovu, aliporudi Dar alimuelezea kijana wake ambaye naye aliliwasilisha ofisini na sisi tukamtuma kazi huku ili achunguze na kuleta taarifa sahihi ili tujue la kufanya. Na ndicho leo kilichofanyika.

Mimi nimezungumza sana, sasa namuachia kipaza sauti mwenyewe kwa sababu amesimama sana. Adel sasa zungumza na umati huu, unataka kujua nini ulikuwa unafanya tangu ulipofika hapa hadi kufanikisha kukamatwa kwa Usonzo."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SIMBA, M-BET WAFURAHIA USHIRIKIANO WA UDHAMINI

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri ya M-BET na Simba zimefurahishwa na utekelezaji wa mkataba wa udhamini ambao ulianza Agosti Mosi, mwaka jana imeelezwa.

**Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Masoko wa M-BET Tanzania, Allen Mushi, katika mkutano mfupi wa utambulisho wa Ofisa Mtendaji Mkuu mpya wa klabu ya Simba Imani Kajula.**

Kajula alifanya ziara maalum kwenye ofisi za kampuni hiyo ikiwa ni mara yake ya kwanza tangu kuchaguliwa kuongoza Simba akichukua nafasi iliyoachwa na, Barbara Gonzalez.

"Utekelezaji wa masharti ya mkataba unafuatwa na tunapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa mashabiki, wanachama na wadau wa soka kwa ujumla. Tunafurahia kushirikiana na Simba," alisema Mushi.

Naye Kajula alisema Simba inajisikia faraja kubwa kufanya kazi na M-BET Tanzania ambao ndio wadhamini wakuu na wadhamini wengine waliopo katika klabu hiyo.

Kajula alisema wataendelea kudumisha ushirikiano huu ambapo umeleta tija kwa klabu yao na kuendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali.

Mbali ya Mushi na Kajula, wengine waliokuwapo katika mkutano huo ni Mkurugenzi Mtendaji wa M-Bet Tanzania, Dhiresh Kaba, Mkurugenzi wa Utawala wa M-BET, Fernando Perez na maofisa wengine wa Simba.

M-BET na Simba zilisaini mkataba wa miaka mitano ambao unaifanya kampuni hiyo kuwa wadhamini wakuu.

Katika mkataba huo, Simba itakuwa inapokea kiasi cha Sh bilioni 4.67 kwa mwaka wa kwanza ambapo mwaka wa pili itapokea sh. bilioni 4.925 na mwaka wa tatu sh. bilioni 5.205.

Pia Simba itakuwa inapokea Sh. bilioni 5.514 kwa mwaka wa nne wa udhamini huo na mkataba wao utahitimishwa na kitita cha Sh. bilioni 5.853 na kufanya jumla ya udhamini wao kipindi cha miaka mitano kuwa Sh. bilioni 26.1.

M-BET pia iliingia mkataba wa miaka miwili na klabu hiyo wenye thamani ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya Simba Queens inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya M-Bet Tanzania, Dhiresh Kaba (wa pili kushoto), akimsikiliza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula (wa nne kulia) katika mkutano mfupi uliofanyika kwenye ofisi za kampuni hiyo jijini, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Azam, Dodoma Jiji hapatoshi

**Na Adam Fungamwango**

SIKU saba tu baada ya kuchapwa mabao 4-1 na Azam FC katika mechi ya hatua ya 32 bora ya mashindano ya Kombe la FA, Dodoma Jiji leo itakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Jamhuri kuwakaribisha wababe wao kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikipania kulipiza kisasi.

Wakati Azam ikihitaji pointi tatu ili kuzifukuza timu zilizo juu ya msimamo wa ligi hiyo kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao, Dodoma Jiji inazihitaji ili isishuke daraja.

Kaimu Ofisa Habari wa Azam, Hasheem Ibwe, aliliambia gazeti hili timu yake inatambua mechi hiyo itakuwa ngumu na ndiyo maana wamekwenda Dodoma mapema ili kuendelea na maandalizi.

"Tumefanya maandalizi mazuri, tunajua mechi itakuwa ngumu kwa sababu siku si nyingi tuliwafunga katika mechi ya Kombe la FA, hivyo hawatakubali kupoteza kirahisi, lakini sisi tunaamini uimara wa kikosi chetu," alisema Ibwe.

Naye Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji, Kassim Liogope, alisema mechi hiyo itakuwa na upinzani, lakini wamejiwekea malengo ya kuibuka na pointi zote tatu katika mechi zao tano zilizobaki ambazo watacheza nyumbani.

"Mashabiki wasikate tamaa, tunakwenda kufanya vyema katika mechi yetu dhidi ya Azam FC, tuko tayari, Azam ni timu nzuri, kwetu mechi itakuwa ya ushindani, malengo tuliyoweka ni kushinda mechi zote zote tano zilizosalia kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma ikiwamo ya kesho (leo)," alisema Liogope.

## Tanzania kicheko Ligi Kuu iking'ara

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imefurahishwa na hatua ya Ligi Kuu Bara kushika nafasi ya tano katika ubora wa ligi za barani Afrika, imefahamika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema kutajwa huko kunaonyesha utawala bora, uwazi na weledi unaosimamiwa kwa pamoja kati ya Shirikisho na Mpira wa Miguu Nchini (TFF) na bodi hiyo.

Shirikisho la Kimataifa la Historia na Takwimu za Mpira wa Miguu (IFFHS), juzi limeitangaza Ligi Kuu Tanzania Bara kushika nafasi ya tano kwa ubora barani Afrika na ya 39 duniani kwa mwaka 2022.

"Kwetu sisi ni kitu kikubwa, hatukufika hapo kwa bahati mbaya ila ni kwa juhudi kubwa za pamoja, za wadhamini, klabu, kampuni zinaounga mkono klabu, waandishi wa habari wanaoisemea ligi yetu, udhamini, mashabiki, tunachukua fursa hii kujipongeza sote. Changamoto sasa ni kuendelea kulinda nafasi iliyopo, isiteremke, iwe hapo au ipande watakapoitangaza msimu ujao," alisema Kasongo.

Aliongeza siku zote namba haziongopi, kwani ni zoezi lililofanyika kisayansi na taasisi ya kimataifa, na yeye kama mtendaji anaona ni sahihi kama chombo hicho kilivyobainisha.

## Galiatano, Alkasusu ulingoni Februari 25

**Na Saada Akida**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Ismail Galiatano anatarajia kupanda ulingoni kuzichapa dhidi Muksini Swalehe 'Alkasusu' katika pambano litakalofanyika Februari 25, mwaka huu Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Pambano hilo litakuwa la raundi 10 na limepewa jina la 'Usiku wa Kisusio', litafanyika kwenye Ukumbi wa YMCA uliopo Moshi.

Galiatano anarejea ulingoni baada ya kutopigana tangu Julai, mwaka jana alipomchakaza Buda Chikoko kutoka Malawi wakati Alkasusu kutoka Naccoz Gym mara ya mwisho alipanda jukwaani Desemba, mwaka juzi dhidi ya Cosmas Cheka ambaye alimchapa kwa pointi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Galiatano, alisema yuko tayari kumkabili Alkasusu na kwa maandalizi aliyoyafanya anaamini anaenda kuendeleza rekodi ya kuibuka na ushindi.

"Ngumi ndio kazi yangu, na lengo langu ni kutoa burudani kwa mashabiki wangu na kuwafanya wafurahi ndio maana najifua ili niweze kupata ushindi na kuendelea kuifanya rekodi yangu kuwa safi," alisema Galiatano.

## ZISIKUPITE

### MARTINELLI KUZEEKEA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Martinelli, mwenye umri wa miaka wa 21 amesaini mkataba mpya na Arsenal ambao utamweka katika klabu hiyo hadi msimu wa joto wa mwaka 2027. (***Athletic***)

### NEWCASTLE YAMTAKA BELLINGHAM

KLABU ya Newcastle United imeripotiwa kujiunga na mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 kutoka Borussia Dortmund msimu wa joto. (***Football transfer***)

### FIORESTINA YAMTAJA AMRABAT

KLABU ya Fiorentina iliachwa ikiwa imechanganyikiwa baada ya mmliki wa Chelsea, Todd Boehly kuchukua jukumu la kujaribu kumsajili kiungo wa kati wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 26, kwa mkopo siku ya mwisho ya uhamisho. (***New York Times***)

### FERNANDEZ AITAJIRISHA PLATE

RIVER Plate inatazamiwa kupokea pauni milioni 28 kufuatia kuhama kwa kiungo wa kati wa Argentina mwenye umri wa miaka 22, Enzo Fernandez, kutoka Benfica kwenda Chelsea. (***Fabrizio Romano***)

### DEULOFEU ALIKARIBIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ilikuwa imekaribia kukamilisha uhamisho wa mshambuliaji wa Hispania, Gerard Deulofeu mwenye umri wa miaka 28 kabla ya mchezaji huyo wa Udinese kuondolewa uwanjani kwa msimu uliosalia Januari kutokana na jeraha la goti. (***Fabrizio Romano***)

### WAKALA AISHANGAA BRIGHTON

WAKALA wa Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21 ameikosoa Brighton kwa kumnyima kiungo huyo wa Ecuador kuhamia Arsenal na kusema fursa hiyo "huenda isipatikane tena maishani". (***Marca90***)

### HARRISON, LEEDS KIMEELEWEKA

WINGA wa Timu ya Taifa ya England, Jack Harrison mwenye umri wa miaka 26 anatarajiwa kusaini mkataba ulioboreshwa katika klabu ya Leeds United katika wiki zijazo. (***Sky Sports***)

### ISCO ASAKA KLABU

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Hispania, Isco mwenye umri wa miaka 30, bado anatafuta klabu mpya na amepewa ofa na timu kadhaa za Ligi Kuu England kwa mkataba wa muda mfupi. (***90min***)

### JUVE KUMWACHA POGBA

JUVENTUS inafikiria uwezekano wa kumuuza au kuvunja mkataba na winga wa Mfaransa, Paul Pogba mwenye umri wa iaka 29. (***Mail***)

### GIROUD KUULA MILAN

STRAIKA wa Ufaransa, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 36, anatarajiwa kuongeza mkataba wake na AC Milan hadi mwaka 2024. (***Sport.Sky***)

### MNIGERIA KUINUNUA SHEFFIELD

BILIONEA wa Nigeria, Dozy Mmobuosi anakaribia kukamlisha ununuzi wa klabu inayoshiriki Ligi ya Championship ya England, Sheffield United kwa pauni milioni 90. (***Times***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AWAZA KUCHEZA KOMBE LA DUNIA 2026

## Mshambuliaji huyo aweka wazi uamuzi huo ingawa...

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi hajaondoa uwezekano wa kuichezea Argentina katika fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2026, lakini alikiri umri utafanya iwe ngumu kushiriki mashindano hayo.

**Messi, ambaye atatimiza umri wa miaka 39 wakati wa fainali zijazo za Kombe la Dunia, mwaka jana alise ma mashindano ya 2022 nchini Qatar yangekuwa ya mwisho kwake.**

Hata hivyo, huku Argentina ikiwa imetwaa taji hilo Desemba, Messi sasa amependekeza yuko tayari kushiriki mashindano yajayo yatakayofanyika Marekani, Canada na Mexico.

"Kwa sababu ya umri itakuwa ngumu kufikia 2026," alisema Messi akiiambia Diario Olé.

"Ninapenda kucheza mpira wa miguu na huku nikijihisi niko katika hali nzuri na kufurahia hili, nitaendelea nalo. Inaonekana ni muda mrefu hadi kombe lijalo la Dunia, lakini inategemea jinsi maisha yangu yanavyoendelea."

Kutiwa moyo kwa Messi kucheza fainali hizo pia kumetoka kwa kocha wa Argentina, Lionel Scaloni.

"Nadhani Messi anaweza kufuzu kwa Kombe lijalo la Dunia," Scaloni aliiambia redio ya Hispania, Calvia FM mwezi uliopita.

"Itategemea sana kile anachotaka na kile kitakachotokea baada ya muda, anajisikia vizuri. Milango itakuwa wazi daima. Ana furaha uwanjani, na kwetu itakuwa vizuri."

Baada ya kupoteza fainali mwaka wa 2014, Messi hatimaye alitwaa taji la Kombe la Dunia baada ya Argentina kuishinda Ufaransa katika mechi ya fainali.

Messi tayari anashikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi za Kombe la Dunia baada ya kumpita Mjerumani, Lothar Matthaus kwa kucheza mechi 26 katika ushindi mnono wa fainali ya 2022.

Pia ni mmoja wa wachezaji watano pekee walioingia uwanjani katika michuano mitano tofauti ya Kombe la Dunia.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,072,5
MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
NAMUNGO
1 | 1.18
X | 3.93
2 | 8.79
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GREENWOOD AFUTIWA MASHTAKA

**MANCHESTER,** England

WINGA wa Manchester United, Mason Greenwood, amefutiwa mashtaka ya unyanyasaji kingono yaliyokuwa yanamkabili katika Mahakama ya Jiji la Manchester.

Greenwood ambaye amekaa nje ya uwanja kwa takribani mwaka mmoja sasa amefutiwa mashtaka hayo juzi na kuachiwa huru.

Winga huyo alikua anatuhumiwa kumfanyia vitendo vya unyanyasaji wa kingono aliyekua mpenzi wake.

Winga huyo ambaye alikua anaanza vizuri ndani ya kikosi cha United alikumbwa na tuhuma hizo dhidi ya mpenzi wake mwishoni mwa mwaka 2021, kitendo kilichofanya kukakaa nje ya uwanja kwa muda wote akishughulika na kesi yake.

Greenwood alitolewa kwenye kikosi cha United pamoja na makampuni mbalimbali ambayo yalikua yamesaini mkataba na mchezaji huyo yakavunja ikiwamo kampuni ya vifaa vya michezo ya Nike.

Nyota huyo alipitia changamoto nyingi baada ya kukumbwa na tuhuma za kumfanyia unyanyasaji mpenzi wake.

# Nunez atamani mafanikio ya Suarez

**LIVERPOOL,** England

DARWIN Nunez ana imani anaweza kufuata nyayo za Luis Suarez pale Liverpool na kwa mafanikio makubwa katika msimu wake wa pili.

Mshambuliaji huyo wa Uruguay amekuwa na wakati mgumu tangu alipowasili Anfield kutoka Benfica Juni mwaka jana, akifunga katika mechi zake mbili za ufunguzi, lakini amefunga mabao nane pekee kwenye michezo 23 aliyocheza.

Ingawa anatambua matatizo ambayo amekumbana nayo katika kipindi cha msimu wake wa kwanza katika soka la England, Nunez anatambua mwanzo mwepesi wa Suarez akiwa Merseyside hapo na anahisi anaweza kurejea kwa mtindo kama huo.

Mshambuliaji wa zamani wa Ajax, Suarez alifunga mabao 15 pekee katika mechi 44 za Ligi Kuu England katika msimu wake wa kwanza na nusu akiwa Liverpool, kabla ya kufunga mabao 54 katika mechi 66 na baadaye kwenda Barcelona mwaka 2014.

"Ni wazi, bado nina mambo mengi ya kufanyia kazi, kwa mfano umaliziaji wangu. Lakini nadhani jambo lile lile linatokea kwangu kama lilivyotokea kwa Suarez. Katika mwaka wake wa pili," amesema Nunez akiambia Sky Sports.

"Kitu kama hicho kilinitokea tayari nikiwa Benfica. Mwaka wa kwanza ulienda vibaya sana kwangu na wa pili ndio mambo yakawa mazuri.

"Hapa, nadhani jambo lile lile linafanyika. Natumaini msimu ujao utakuwa hivyo. Nitaweka uwezo wangu bora mbele na natumaini nitapata bahati kidogo."



549,524/-

# DABO KOMBINESHENI ZAMPA DONGE JACKPOT BONUS SHABO

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYAKAZI wa Nyakato, Mwanza, Merick Shabo wiki iliyoisha ameondoka na kitita kinono cha Sh. milioni 16.4 cha bonus ya Jackpot ya kati kati ya wiki baada ya kupatia kwa usahihi mikeka mitatu ya Jackpot.

Akizungumza katika ofisi za SportPesa Oysterbay jijini Dar-Es-Salaam, Merick alisema alianza kucheza na SportPesa miaka mitano iliyopita baada yeye kufuatilia mashindano ya Kombe la SportPesa.

"Mimi ki ukweli nilivutiwa kuanza kuifuatilia na kucheza na SportPesa wakati ule mashindano ya kwanza ya SportPesa Cup yalipoanza. Mimi ni shabiki mkubwa wa Yanga na napenda soka hivyo baada ya yale mashindano kuanza nilikuja kujua waandaaji na wadhamini ni SportPesa ndipo nilipojua kuhusiana na huduma zao na kujisajili kupitia rafiki yangu, ambaye sitamtaja jina".

Kuhusu fedha nono aliyoshinda ya Sh. milioni 16.4, alisema katika mkeka wa Jackpot aliyocheza wiki iliyopita aliweka mkeka wenye dabo kombinesheni tano ambapo kati ya hiyo mikeka mitatu ndiyo iliyompa ushindi wa nguvu.

"Mimi niliweka jumla ya mikeka 10, lakini hiyo mikeka mitatu ndio iliyonipa pesa. Unajua siku ya Jumatatu niliweka mikeka mitano ya kwanza ambayo yote ilikuwa na dabo kombinesheni. Baada ya hapo niliweka mikeka mingine mitano ya nyongeza, niliyocheza bila dabo kombinesheni"

"Nichukue fursa hii kuwashukuru SportPesa kwa fursa ya Jackpot bonus na malipo ya papo hapo. Unajua Jackpot za SportPesa haushindi tu kiasi halisi cha Jackpot lakini sisi tunaocheza tunapata fedha kupitia bonus.

Ni jambo la kushukuru sana. Nadhani unaona bonus niliyopata kwa kiasi kikubwa ni zaidi ya hata baadhi ya Jackpot za makampuni mengine. Cha pili mimi niliposhinda ilikuwa majira ya saa 5 asubuhi, ambapo nilikuwa kazini naendelea na shughuli zangu kama kawaida, nilishtukia sms tatu za kunipongeza kwa kushinda Jackpot bonus ya jumla ya Sh 16,496,192.

Merick anasema katika kiasi hiki cha fedha alichopata atampatia mama yake fungu la kumi na nyingine atawekeza kwenye mipango yake, ambayo hakutaka kuweka wazi kwa sasa.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Kampuni ya SportPesa, Sabrina Msuya, alimpongeza Merick kwa ushindi mnono na kuwakumbusha Watanzania, SportPesa ndio mahala sahihi na penye urahisi wa kuondoka na mkwanja.

Moja kati ya ahueni ni hii dabo kombinesheni. Katika Jackpot ya kati kati ya wiki ambayo inakuwa na jumla ya mechi 13. Mchezaji amepewa nafasi ya kuweka dabo kombinesheni saba. Hii ina maana mchezaji unabakiwa na mechi tano za kuumiza kichwa.

Merick alishinda dabo kombinesheni tatu ambapo ya kwanza ilikuwa dabo kombinesheni ya mechi 12 kati ya mechi 13. Hii ilimlipa Sh. milioni 9.8 na ya pili alishinda dabo kombinesheni ya mechi 11 kati ya mechi 13. Hii ilimlipa Sh. milioni 5.3 na nyingine ilikuwa na kombinesheni ya tatu ilikuwa ya mechi 10 kati ya 13 na ilimlipa Sh. milioni 1.3.

Sabrina anamalizia kwa kusema ahueni ya pili inayopatikana SportPesa pekee ni kupitia Quick Pick. Hii ni huduma ambayo inamsaidia mchezaji anayecheza Jackpot kucheza kwa haraka, na mchezaji haitaji ujuzi wa kujua sana kucheza au kuchambua.

"Unachotakiwa kufanya ni Kwenda kwenye kurasa ya Jackpot iwe ya katikati ya wiki au Supa Jackpot. Baada ya hapo unabonyeza kitufe kilichoandikwa Quick Pick na timu zinajipanga kwa machaguo tofauti".

Supa Jackpot ya wiki imesimamia Sh. 1,072,549,524.





## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/02/23 | 18:00 | Preston North End vs Bristol City | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 02. 04/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Queens Park Rangers | 3.00 | 3.20 | 2.39 |
| 03. 04/02/23 | 18:00 | Reading FC vs Watford FC | 2.70 | 3.20 | 2.60 |
| 04. 04/02/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KVC Westerlo | 2.75 | 3.45 | 2.41 |
| 05. 04/02/23 | 22:00 | FC Emmen vs Vitesse Arnhem | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 04/02/23 | 23:00 | Excelsior Rotterdam vs RKC Waalwijk | 2.70 | 3.35 | 2.49 |
| 07. 04/02/23 | 23:00 | Stade Rennes vs Lille OSC | 2.30 | 3.35 | 2.95 |
| 08. 04/02/23 | 23:30 | Estoril Praia vs Vitoria SC Guimaraes | 2.65 | 3.00 | 2.75 |
| 09. 05/02/23 | 03:30 | Atletico Lanus vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.31 | 2.85 | 2.80 |
| 10. 05/02/23 | 03:30 | Argentinos Juniors vs Racing Club Avellaneda | 2.60 | 2.70 | 2.60 |
| 11. 05/02/23 | 15:30 | Royal Antwerp FC vs Club Brugge | 2.49 | 3.40 | 2.65 |
| 12. 05/02/23 | 16:00 | Villarreal CF B vs Granada CF | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 13. 05/02/23 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.49 | 3.15 | 2.37 |
| 14. 05/02/23 | 16:30 | Go Ahead Eagles vs NEC Nijmegen | 2.40 | 3.35 | 2.85 |
| 15. 05/02/23 | 17:00 | Nottingham Forest vs Leeds United | 2.60 | 3.30 | 2.60 |
| 16. 05/02/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs FC Nantes | 2.65 | 3.10 | 2.70 |
| 17. 05/02/23 | 17:00 | Torino FC vs Udinese Calcio | 2.24 | 3.20 | 3.25 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 04/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2951 | Gor Mahia vs Nairobi City Stars FC | 1.61 | 3.48 | 5.20 |
| 15:30 | 4558 | Norwich City vs Burnley | 2.48 | 3.28 | 2.68 |
| 15:30 | 4707 | Rotherham vs Sheffield Utd | 4.57 | 3.77 | 1.68 |
| 15:30 | 4715 | Everton vs Arsenal | 6.86 | 4.17 | 1.44 |
| 16:00 | 1322 | Sivasspor vs Besiktas | 3.34 | 3.39 | 2.08 |
| 16:00 | 2615 | Espanyol vs Osasuna | 2.45 | 2.99 | 3.04 |
| 16:30 | 3734 | Chippa Utd vs Stellenbosch | 2.78 | 2.94 | 2.63 |
| 16:30 | 4939 | Orlando Pirates vs Mamelodi Sundowns | 4.00 | 3.27 | 1.91 |
| 16:30 | 5527 | Golden Arrows vs Bloemfontein Celtic | 2.41 | 3.06 | 2.95 |
| 17:00 | 2921 | Cremonese vs Lecce | 2.59 | 2.99 | 2.79 |
| 17:30 | 1325 | Eintracht Frankfurt vs Hertha BSC | 1.46 | 4.46 | 5.94 |
| 17:30 | 1719 | FC Koln vs RB Leipzig | 3.61 | 3.56 | 1.92 |
| 17:30 | 3019 | VfL Bochum vs Hoffenheim | 2.72 | 3.41 | 2.38 |
| 17:30 | 3197 | Borussia Dortmund vs SC Freiburg | 1.64 | 3.98 | 4.57 |
| 17:30 | 4632 | Wydad Casablanca vs Al Hilal Riyadh | 2.54 | 3.06 | 2.64 |
| 17:30 | 4810 | Union Berlin vs Mainz | 1.94 | 3.27 | 3.86 |
| 18:00 | 1789 | Hull City vs Cardiff | 2.16 | 3.21 | 3.26 |
| 18:00 | 2291 | Manchester Utd vs Crystal Palace | 1.42 | 4.25 | 7.02 |
| 18:00 | 2472 | Wolverhampton vs Liverpool | 3.77 | 3.62 | 1.86 |
| 18:00 | 2605 | Swansea vs Birmingham | 1.85 | 3.47 | 3.96 |
| 18:00 | 3343 | Middlesbrough vs Blackpool | 1.52 | 4.05 | 5.72 |
| 18:00 | 3407 | Millwall vs Sunderland | 2.07 | 3.26 | 3.46 |
| 18:00 | 4089 | Reading vs Watford | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 18:00 | 4330 | Huddersfield vs QPR | 2.96 | 3.15 | 2.36 |
| 18:00 | 4840 | Brighton vs Bournemouth | 1.33 | 4.96 | 7.94 |
| 18:00 | 5398 | Brentford vs Southampton | 1.83 | 3.50 | 4.05 |
| 18:00 | 5718 | Aston Villa vs Leicester | 1.94 | 3.47 | 3.62 |
| 18:00 | 5776 | Preston vs Bristol City | 2.37 | 3.16 | 2.92 |
| 18:00 | 5794 | Luton Town vs Stoke City | 2.19 | 3.21 | 3.21 |
| 18:15 | 5814 | Elche vs Villarreal | 4.80 | 3.75 | 1.68 |
| 18:30 | 2719 | SuperSport Utd vs Cape Town City | 2.09 | 3.11 | 3.58 |
| 18:30 | 2884 | Santa Clara vs Boavista | 2.54 | 2.99 | 2.89 |
| 18:30 | 4866 | Young Africans vs Namungo | 1.18 | 3.93 | 8.79 |
| 19:00 | 4311 | Antalyaspor vs Gaziantep BB | 1.95 | 3.50 | 3.61 |
| 19:00 | 4684 | Paris St Germain vs Toulouse | 1.34 | 5.15 | 7.36 |
| 20:00 | 1743 | Roma vs Empoli | 1.45 | 4.14 | 6.71 |
| 20:30 | 1923 | Seattle Sounders vs Al Ahly Cairo | 2.44 | 3.12 | 2.70 |
| 20:30 | 2575 | Monchengladbach vs Schalke 04 | 1.50 | 4.46 | 5.35 |
| 20:30 | 3661 | Atletico Madrid vs Getafe | 1.40 | 4.11 | 8.81 |
| 20:30 | 4417 | Newcastle vs West Ham | 1.59 | 3.70 | 5.53 |
| 20:30 | 5567 | Dodoma FC vs Azam | 3.50 | 4.00 | 1.40 |
| 21:00 | 2379 | Troyes vs Lyon | 4.28 | 3.93 | 1.70 |
| 21:00 | 4375 | Marumo Gallants FC vs Sekhukhune United | 2.57 | 2.84 | 2.95 |
| 21:00 | 5365 | Benfica vs Casa Pia Atletico | 1.18 | 6.36 | 13.91 |
| 22:30 | 1618 | Algeria vs Senegal | 1.85 | 3.20 | 4.60 |
| 22:30 | 3047 | St. Gallen vs Servette Geneva | 1.93 | 3.56 | 3.61 |
| 22:45 | 2867 | Sassuolo vs Atalanta | 3.51 | 3.66 | 1.92 |
| 23:00 | 4926 | Betis vs Celta Vigo | 2.22 | 3.10 | 3.35 |
| 23:00 | 5871 | Rennes vs Lille | 2.27 | 3.28 | 3.03 |
| 23:30 | 1257 | GD Estoril vs Vitoria Guimaraes | 2.63 | 2.98 | 2.78 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


## Yanga, Namungo hesabu zitaamua

INATOKA UK 24

kushindana, tumeondolewa katika Kombe la Shirikisho (ASFC), hilo tumesahau, tunaingia na mipango mipya katika mchezo huo kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Nsajigwa.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Dodoma Jiji dhidi ya Azam FC na Geita Gold watawaalika Coastal Union kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nyankumbu iliyoko mkoani Geita.

## Kajula: Makombe kurejea Simba SC

INATOKA UK 24

hao watashuka tena dimbani kesho kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan, timu zote zikitumia mchezo huo kujiimarisha kuelekea mechi za kimataifa.

Ikiwa hapa nchini, Al Hilal imecheza mechi nyingine za kirafiki dhidi ya Namungo na Azam.

Michezo
Nipashe Jumamosi Februari 4, 2023



Messi awaza kucheza Kombe la Dunia 2026 UKURASA 21

# Yanga, Namungo hesabu zitaamua

## ●●● Kaze afunguka kubadilisha mfumo kutokana na historia ya...

**Na Saada Akida**

MBIO za kuwania ufalme wa soka nchini zinatarajia kuendelea tena kwa Yanga kuwakaribisha Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mechi hiyo Yanga itawakosa wachezaji wake wawili, Denis Nkane na Abdultwalib Mshery, ambao wanaendelea na matibabu lakini taarifa njema ni kurejea kwa kiungo wao wa kimataifa raia wa Uganda, Khalid Aucho.

Mabingwa watetezi, Yanga watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi mnono wa mabao 7-0 walioupata dhidi ya Rhino Rangers inayoshiriki Ligi Daraja la Pili katika mchezo wa hatua ya 32 Bora ya mashindano ya Kombe la FA (ASFC).

Namungo yenyewe itawakabili Yanga huku ikiwa na kumbukumbu mbaya ya kutolewa katika michuano ya FA na Ihefu ya Mbeya.

Kuelekea mchezo mchezo huo Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kwa ajili ya kupambana ili kuvuna pointi tatu muhimu na kujiimarisha zaidi katika mbio za kutetea ubingwa wanaoushikilia.

**Kaze alisema wamepata muda mzuri wa kujiandaa mchezo huo na wachezaji wao wanatambua umuhimu wa kuendeleza kasi ya ushindi na kukumbuka historia yao wanapokutana na Namungo FC.**



Mshambuliaji wa Azam FC, Ayoub Lyanga, akifanya mazoezi kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji Dodoma Jiji unaotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

"Tunaamini tumejiandaa kimbinu na kisaikolojia kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo, historia ya mechi tunapokutana inakuwa ngumu sana, Namungo inacheza vizuri, mechi ya kwanza tulipata ushindi lakini kuna mambo mengi yamebadilika kwa sasa, wana kocha mpya na wameongeza wachezaji katika kipindi cha dirisha dogo, sasa hivi inafanya vizuri na mchezo wao mwisho wa Ligi Kuu walimfunga KMC, wamekuwa na morali kubwa katika mchezo wetu," alisema Kaze.

Mwakilishi wa wachezaji wa Yanga, Ibrahim Baka, alisema wamefanya maandalizi mazuri na wako tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi kama walivyofanya mechi zilizopita.

"Kila kitu makocha wamemaliza kazi kubwa iliyobaki ni kwetu kufanya kazi, mchezo utakuwa mgumu na presha kubwa kutokana na kila mmoja wetu kuhitaji matokeo, ila kwetu sisi Yanga pointi tatu muhimu sana," alisema Baka.

Naye Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Shandrack Nsajigwa, alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani na ngumu kwa sababu wapinzani wao wako vizuri na wamejiandaa kiufundi.

Nsajigwa alisema wamejianda kuhakikisha wanazuia na kushambulia kwa umakini ili warejee nyumbani kwao Lindi wakiwa wamevuna pointi hizo muhimu na wataingia dimbani wakiwa na mipango mingine tofauti na walivyocheza mechi iliyopita.

"Tumeandaa vizuri timu yetu

INAENDELEA UK 23

# Kajula: Makombe kurejea Simba SC

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi kinatarajia kuondoka nchini Jumatano kuelekea Guinea kwa ajili ya mchezo wa hatua ya makundi wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC utakaopigwa Febuari 10, mwaka huu nchini humo, bosi mpya wa Simba, Imani Kajula, amesema anaamini watarejesha mataji yaliyopotea msimu uliopita.

Kajula ambaye amerithi mikoba iliyoachwa na Barbara Gonzalez, alisema hayo juzi jioni baada ya kukutana na wachezaji wa Simba kwa mara ya kwanza.

Ofisa Mtendaji huyo aliwaambia wachezaji wa timu hiyo kudumisha nidhamu ndani na nje ya uwanja na kwa kufanya hivyo watafikia malengo ya kufanya vizuri katika michezo yote iliyopo mbele yao ikiwamo mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Aliwaambia wachezaji watakapojituma na watakaposhirikiana vyema na viongozi walioko katika benchi la ufundi, hakika watavuna kile wanachokihitaji na si vinginevyo.

Alisema mafanikio hupatikana mahali kwenye umoja na mshikamano ambao pia huzalisha furaha.

"Nimefurahi kukutana nanyi na kuongea mambo machache, kikubwa nawasisitiza furaha ya wanasimba ipo miguuni kwenu. Tunahitaji kurejesha mataji pamoja na kufanya vizuri kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hilo litawezekana endapo wachezaji mtatimiza majukumu yenu uwanjani," Kajula alisema.

Aliongeza menejimenti itahakikisha wanapata kila kitu wanachostahili kwa wakati ili kazi yao iwe kufikiria uwanjani na kujituma katika michuano yote wanayoshiriki.

Baada ya mechi ya jana usiku dhidi ya Singida Big Stars, Wekundu wa Msimbazi

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >